# Nipashe

Ijumaa Januari 15, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580461

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Ukurasa 12

Kuyumba soko la nyanya kuvuka mpaka kunavyowaacha taabani wauzaji Tarime

BUFE

IJUMAA JANUARI 15, 2021 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14

MGOGORO MPAKA ZAMA 1952...

Waziri azuru hifadhini Kilombero akimaliza msuguano na wananchi

DED Mkuranga ajinasibu na stendi Sh. bil. 50, mwendokasi ina egesho

Na Yasmine Protace, MKURANGA

UKURASA 11

**MBARONI** tuhuma kuuziana dhahabu wakiwa 'gesti'

UKURASA 4



**DED** asimamishwa kwa kuweka vibaya mwili wa marehemu

UKURASA 8

# Wenyeviti vitongoji waswekwa mahabusu

UKURASA 2



UKURASA WA 5

## MLINZI MBARONI TUHUMA ZA MAUAJI YA MKE WAKE

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linamshikilia mfanyakazi wa kampuni ya ulinzi ya Komesha, Shabani Mpacha, kwa tuhuma za kumuua mke wake kwa madai ya...

UKURASA WA 4

## WAWILI MBARONI WAKIDAIWA KUJIFANYA ASKARI POLISI

JESHI la Polisi Temeke limewakamata watu wawili wanaotuhumiwa kuwa ni askari 'feki' wanaodaiwa kutumia kofia ya jeshi hilo kuwatishia, kuwalaghai wananchi na kuwaibia mali zao. Akielezea mbele ya...



Rais John Magufuli akimkaribisha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, alipowasili Ikulu ndogo ya Chato, mkoani Geita jana. Katikati ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA NA IKULU**

# Magufuli amwita Maalim Seif shujaa

UKURASA 2

# Msaidizi wa Hayati Askofu Banzi naye afariki dunia

UKURASA 2

**MICHEZO** **KAZE: TULIISHIKA SIMBA** UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

## Msaidizi wa Askofu Banzi afariki dunia

**Na Waandishi Wetu,** TANGA

SIKU chache baada ya aliyekuwa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Tanga, Antony Banzi, kufariki dunia, kanisa hilo limepata pigo tena baada ya kuondokewa na aliyekuwa msaidizi wa askofu, Padri Martin Maganga.

Padri Maganga alifariki dunia juzi Mwanga mkoani Kilimanjaro baada ya hali yake kiafya kubadilika ghafla, alipokuwa akitokea kwenye matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, mjini Moshi.

Kifo hicho kimeonekana kuwashtua watu wengi kutokana na padri huyo kuwa na afya njema alipokuwa akisimamia taratibu za mazishi ya Askofu Banzi wiki mbili zilizopita.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mazishi, Padri Thomas Msagati, alisema mwili wa Padri Maganga umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga, Bombo.

Padri Msagati alisema mazishi yanatarajiwa kufanyika Januari 19, mwaka huu, katika sehemu maalumu ya kuzikia mapadri, Parokia ya Kilole, Korogwe mkoani Tanga.

"Baada ya kuwasiliana na Msimamizi Mkuu wa Jimbo, Padri Kiangio na Askofu (Mkuu Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Judathedeus Ruwa'ichi, ilionekana kwamba tutazika siku ya Jumanne huko Korogwe," alisema Padri Msagati.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, mara ya mwisho tatizo lililokuwa likimsumbua marehemu ni kisukari pamoja na ugonjwa wa moyo, hivyo kulazimika kufanya kliniki KCMC.

Wakati wa uhai wake, Padri Maganga, alikuwa akihudumu pia kama Paroko katika Parokia ya Mtakatifu Theresia, Barabara ya 20 jijini Tanga.

Aliteuliwa kuwa Makamu wa Askofu Banzi mwaka 2008 na hadi anafikwa na umauti, alikuwa amehudumu katika wadhifa huo kwa miaka 12.

Pia amewahi kuwa Mkufunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) kilichoko jijini Mwanza.

**●Imeandikwa na Boniface Gideon na Lulu George**

# RC asweka ndani wenyeviti vitongoji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ameagiza wenyeviti 21 wa vitongoji katika Mji Mdogo wa Mikumi wilayani Kilosa, kuswekwa mahabusu kwa kushindwa kuhamasisha wananchi kushiriki ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Mikumi.

Vyumba hivyo vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi 200 ambao ni miongoni mwa waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao, Ole Sanare amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kilosa kuwakamata viongozi hao.

Ole Sanare alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea shule hiyo na kukuta hakuna jitihada zozote zinazofanywa na viongozi hususani kwa wenyeviti wa vitongoji katika Mji Mdogo wa Mikumi katika kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye ujenzi huo.

Shule hiyo imepangiwa wanafunzi 432, lakini wanafunzi 200 wamebainika kukosa vyumba vya madarasa na kuhitajika vyumba vine, ili kuwezesha wanafunzi wote walichaguliwa kupata nafasi.

"Hapa serikali imeleta Sh. milioni 25 lakini haziwezi kutosha, hivyo kinachopaswa ni ushiriki wa nguvu kazi za wananchi. Hili linahitaji uhamasishaji wa wananchi kupitia viongozi waliochaguliwa na wananchi wenyewe, lakini viongozi hapa wamelala tu," alisema.

Ole Sanare alipofika eneo la ujenzi, hakuwakuta viongozi wa vitongoji hao huku ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa ukiwa katika hatua ya msingi wakati zimebaki siku chache kwa shule zote kufunguliwa na wanafunzi kuanza masomo.

Mkuu huyo wa mkoa alifanya ziara hiyo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Mjaliwa, kutaka wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya darasa la saba mwaka jana, kuwa madarasani mara shule zitakapofunguliwa.

Pia alitaka kila mkoa kuhakikisha haukosi vyumba vya madarasa ya kusomea na madawati.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akionyesha kitabu kinachoelezea mafanikio ya miaka mitano ya uongozi wa Rais John Magufuli kinachoitwa "The Game Changer: President Magufuli's First Term in Office" kilichohaririwa na Prof. Tedi Maliyamkono (kulia), baada ya kukizindua jijini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako. **PICHA: OWM**

# Rais Magufuli amwita Maalim Seif shujaa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amesema amemwita Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ni shujaa kutokana na uamuzi aliochukua wa kuungana na serikali.

Pia amesema uamuzi huo ni wa kishujaa na wenye maslahi kwa Wazanzibar wote kwa kuwa umeziunganisha ndoa zilizovunjika.

Kutokana na uamuzi huo, Rais Magufuli amesema anaiona Zanzibar mpya, yenye maendeleo itakayokuwa kama Dubai na kwamba uzoefu wa Maalim Seif unahitajika kwenye uongozi wa sasa.

Alitoa kauli hiyo jana nyumbani Chato, mkoani Geita baada ya kutembelewa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyeambatana na Maalim Seif.

Wakiwa katika mazungumzo, Rais Magufuli alisisitiza ushirikiano kwenye kazi kumwomba Maalim Seif kushirikiana na Dk. Mwinyi kuhakikisha mali za umma zinapewa kipaumbele na kulindwa pamoja na kutohofia 'kutumbua majipu'.

"Rais Mwinyi usiogope kutumbua majipu wanaokwamisha maendeleo. Zanzibar itakuwa kama Dubai. Kukiwa na upendo, amani, kusipokuwapo na rushwa, wawekezaji watakuja. Wananchi wa Zanzibar na Afrika kwa ujumla wanahitaji maendeleo," alisema.

"Mambo ya vyama yasitusumbue, hata Maalim ukitaka kuja kuoa Chato, CCM ruksa. Tunatakiwa Watanzania kutanguliza maslahi ya taifa, mara nyingi maadui wangependa kuona tunagombana. Lakini wameshindwa, viongozi ninyi hamna uamuzi wa kuona umoja unavunjika," aliongeza.

Rais Magufuli alisema kitendo cha viongozi hao kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kimefanya ndoa zilizovunjika kutokana na tofauti za itikadi kisiasa, kuungana tena.

"Kuna ndoa zilivunjika Pemba kwa sababu mwanamke aliipigia kura CCM, mwanamume akakipigia kura ACT-Wazalendo. Siku Maalim alipoingia, ndoa hizo ziliungana, maamuzi (uamuzi) yake (wake) yamewaunganisha (umewaunganisha) wanandoa, maana yake yana (una) baraka kwa mwenyezi Mungu," alisema.

Kutokana na hatua hiyo, Rais Magufuli alisema hivi sasa umefunguliwa ukurasa mpya, hususani katika kufuatilia masuala muhimu kuwasaidia Watanzania.

Rais Magufuli alisema uamuzi wa Maalim Seif ni wa kishujaa una mwelekeo na mwongozo wa Mungu, kwa sababu nchi kadhaa duniani zinashindwa kuendelea kutokana na ugomvi.

"Leo amekuja (Maalim Seif) kufanya kazi na mtoto kwa hiyo uzoefu wa Maalim Seif unahitajika kwa kiasi kikubwa katika uongozi wa sasa. Nilipomtania una umri gani aliniambia ana miaka 77, nilifikiri ana 72," alisema.

"Atakapomaliza uongozi atakuwa na miaka 82. Kwa hiyo 'experience' (uzoefu) yake ni kubwa katika uongozi. Tunamwitaji katika uongozi ndiyo maana nilimpongeza sana kwa maamuzi (uamuzi) yake (wake)."

Rais Magufuli alisema, wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara wanahitaji maendeleo ya kweli, kwamba alimfahamu Rais Mwinyi kwa takribani miaka 20, kwa kuwa ni mchapakazi.

"Bila Zanzibar hakuna Tanzania, bila Zanzibar hakuna Tanzania. Viongozi wote hawa nimewataka waendelee kuchapa kazi, sitawaacha kamwe, sababu wote wanahubiri amani," alisema.

Aidha, Rais Magufuli alisema majadiliano katika kikao chao yalilenga masuala tofauti ikiwamo maendeleo, umoja wa kitaifa pamoja na miradi ya ujenzi.

Rais Mwinyi alisema mazungumzo baina yao yalilenga kujenga nchi, kuwaunganisha Wazanzibar.

Alisema anamshukuru Rais Magufuli kwa dhamira yake ya kuisaidia Zanzibar ikiwamo ombi aliloliwasilisha hivi karibu kwa Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje ya China, Wang Yi, kuomba Dola za Marekani milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 148 za barabara za Zanzibar.

Naye Maalim Seif alisema wamekuwa na mazungumzo mazuri ya namna ya kuwaunganisha Watanzania wote, kwamba amepata matumaini kuona Rais Magufuli ana dhamira ya kuwaunganisha Waunguja na Wapemba.

**●Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Maulid Mmbaga**

## TANGAZO

Tpb Bank
Grow with us

# TPB BANK MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Call Account | 100,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Scout Minor | 10,000 |
| | Scout | 30,000 |
| | WADU | 20,000 |
| | YANGA VIP Card | 1,200,000 |
| | YANGA Member Card | 25,000 |
| | Group Account | FREE |
| Bank Statement | | Within a month it is FREE and more than a month is 1500 per document |
| Monthly Maintenance Fee | Savings Account | 1,560 |
| | Platinum Account | 1,560 |
| | WADU Account | FREE |
| | Call Account | 6,500 |
| | Minor Account | FREE |
| | Group Account | FREE |
| Dormant Accounts Fee | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 years to 10 years | 5,000 |
| | 11 years to 15 years | 10,000 |
| Activation of Dormant Account | | FREE |
| ATM Charges | ATM Balance Enquiry- All cards | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Cash Withdraw on TPB ATMs | 1,300 |
| | Cash Withdraw on other UMOJA SWITCH ATM | 1,300 |
| POS Branches | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | 2,600 |
| POS Agents | Balance Enquiry | 100 |
| | Mini statement | 200 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | see Tiered Fees 1 |
| Mobile Banking | Balance Enquiry | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Full Statement | 400 |
| | Pin Charge | FREE |
| | Notification /Alert | 250 |
| | Account Transfer | FREE |
| | Mobile Agent Deposit | 200 |
| | Mobile Agent Withdraw | see Tiered Fees 2 |
| | Mobile Money to Bank Deposit | 1,300 |
| Closing Account | | 13,000 |
| FDR Min. Opening Balance | | 100,000 |
| ATM Issuance and Replacement Fees | Popote Card | 15,000 |
| | Yanga Member card | 20,000 |

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Other ATM & Normal Card | Pin Re-issue | FREE |
| | Collection of ATM crad at Non Domicile Branch | 6,500 |
| | Uncollected and destroyed ATM card | 6,500 |
| | First ID card (Local and Foreign Currency) | 4,000 |
| | Replacement Of ID card | 2,600 |
| Cash withdraw | Teller withdraw upto 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller withdraw from 10,000,001 to 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller withdraw from 50,000,0001 to 100,000,00 | 15,000 |
| | Teller withdraw above 100,000,001 | 30,000 |
| Cheques Fees | Cheques Clearing Fee | 3,000 |
| | Special Clearance | 50,000 |
| | Dishonoured Cheque | 35,000 |
| Electronic Fund Transfer (EFT) | TISS Inwards | FREE |
| | TISS- Outward | 10,000 |
| Standing Order | Within the Bank | 1,300 |
| | To other Banks | 13,000 |
| POS Withdraw &Money Transfer/ Tiered fees | POS Withdraw | Tiered 1 |
| Tiered 1 | 0-10,000 | 800 |
| | 10,000.01-20,000 | 1,250 |
| | 20,000.01-50,000 | 1,500 |
| | 50,000.01-100,000 | 2,250 |
| | 100,000.01-200,000 | 2,750 |
| | 200,000.01-300,000 | 4,200 |
| | 300,000.01-400,000 | 5,500 |
| | 400,000.01-500,000 | 6,000 |
| | 500,000.01-700,000 | 6,500 |
| | 700,000.01-2,000,000 | 7,500 |
| Tiered 2 | TPB Mobile Transfer Fee | Tiered 1 |
| | 500-10,000 | 850 |
| | 10,000.01-50,000 | 1,200 |
| | 50,000.01-100,000 | 1,500 |
| | 100,000.01-250,000 | 2,800 |
| | 250,000.01-500,000 | 4,600 |
| | 500,000.01 - 750,000 | 7,500 |
| | 750,000.01 - 1,000,000 | 10,000 |

## RATES AND CHARGES FOR USD ACCOUNT

| | | |
|---|---|---|
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| Deposit Fee | Non Account Holder | Free |
| Opening Balance | | 50 |
| Account closure fee | | 10 |
| Bank Statements | | Free |
| | Balance Enquiry- Banking Hall | Free |
| | Confirmation letter | Free |
| Withdraw Fees | Below 50 | 1 |
| | 51-1,000 | 2.5 |
| | 1,001-2,250 | 5 |
| | 2,251-5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25% |
| Cheque | Any amount | 1.3 USD (TZS Equivalent) |
| | Special Clearance | 40 |
| | Unpaid cheque-Refer to Drawer | 10 |
| | Special Payment | 20 |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re- Activation | Free |
| TISS | | 10 |

Tpb Bank
Grow with us

+255 787 669 977 tpbbank//facebook tpbbank//instagram www.tpbbank.co.tz

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

### 1. FEES ON CONSUMER LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved Loan. Minimum TZS. 10,000/= |

### 2. FEES ON WASTAAFU LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 2. | Loan Application Fee | TZS. 10,000/= |
| 3. | Loan Administration Fee | 1.5% Minimum. TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |

### 3. OTHER CHARGES ON INDIVIDUAL MICRO CREDIT

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | MIC Loan Application Fee | TZS. 20,000/= |
| 2. | MIC Loan Processing/Administration Fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |

### 4. INTEREST RATES AND OTHER CHARGES ON BUSINESS LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Loan Application Fees for Business and Personal Loans | TZS. 50,000/= |
| 2. | Loan Administration Fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |



# Mbaroni kwa kuuziana dhahabu 'gesti'

**Na Happy Severine,** BARIADI

JESHI la Polisi Mkoa wa Simiyu linawashikilia watu 15 kwa kosa la kuuziana dhahabu katika nyumba ya kulala wageni katika mgodi wa dhahabu Lubaga, ulioko Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, mkoani humo.

Akiongea na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Richard Abwao, alisema watu hao wamekamatwa Januari 13, mwaka huu, majira ya saa 1:00 jioni wakiwa na madini hayo yenye uzito wa gramu 9.2.

Abwao alisema, watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa kwenye nyumba hiyo ndani ya mgodi huo wakifanya biashara ya kuuzia madini hayo kinyume cha sheria.

"Askari wetu wakiwa doria kwenye mgodi huo, walikuwakuta watu hawa wakifanya biashara hiyo kwenye nyumba ya kulala wageni ambayo ipo ndani ya mgodi huo, sheria inataka biashara ifanyike kwenye soko la madini," alisema Abwao.

"Kwenye mgodi huo kuna soko la madini ambalo limeanzishwa na serikali linalotumika kuuzia madini, lakini hawa walikuwa sehemu ambayo siyo sahihi na lengo lao lilikuwa kukwepa kulipa kodi ya serikali," aliongeza Abwao. Awali, akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa wilaya hiyo, Festo Kiswaga, amelipongeza jeshi hilo kwa kukamata watu hao na kusema hatua kali zitachukuliwa dhidi yao ili iwe fundisho.

Kiswaga alisema serikali iliweka soko kwenye mgodi huo litumike kwa ajili ya kuuzia madini, lakini bado kuna watu wanaendelea kuuziana vichochoroni na kuwataka waache mara moja.

"Vyombo vyote vipo kazini, tutaendelea kuwakamata, tunazo taarifa wapo wengine, tutawakamata wote, niwaombe watu wote kwenye mgodi huo waache mara moja, hatutakuwa na mzaha kwenye hili," alisema Kiswaga.



Watuhumiwa wa kesi ya kuongoza genge la uhalifu na kukutwa na madini bila ya kibali yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 42, wakiwa chini ya ulinzi baada ya kusomewa mashtaka yao Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## Lawyers Environmental Action Team

### Publication of Bi-annual Income and Expenditure.

Lawyers Environmental Action Team is, local Non-Governmental Organization which was found in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with Certificate of Compliance No. 1985.

**Vision:** Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.

**Mission:** To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, the Lawyers Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from July 2020 to December 2020.

**Bi-Annual income and Expenditure for the period from July to December 2020**

| | |
|---|---|
| **Income:** | |
| Receipt from Donors | 736,647,548.56 |
| Bank Interest | 62,341 |
| **Total Income** | **736,709,889.56** |
| **Expenditure:** | |
| Legally empower Urbanites living in Dar es Salaam to access and enforce a right to live in clean environment | 90,025,560.46 |
| Examining the Extractive Legal regime in Tanzania | 28,675,993.68 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | 423,302,459.37 |
| Environmental Advocacy SJRS in Rukwa Tanzania | 182,268,992.40 |
| Human & Admin Resources Activities | 12,436,883.65 |
| **Total expenditure** | **736,709,889.56** |
| **Surplus/Deficit:** | - |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Legal Services Facility (LSF), Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania) and the International Union for Conservation of Nature–Netherlands (IUCN-NL).

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingra Street, Mikocheni B, House No 8,**
**P.O. Box 12605, Dar es Salaam;**
**Email: info @leat.or.tz.**


# Wawili mbaroni tuhuma kujifanya askari polisi

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Temeke limewakamata watu wawili wanaotuhumiwa kuwa ni askari 'feki' wanaodaiwa kutumia kofia ya jeshi hilo kuwatishia, kuwalaghai wananchi na kuwaibia mali zao.

Akielezea mbele ya waandishi wa habari jana namna walivyowanasa watuhumiwa hao, Kamanda wa Polisi Temeke, Amos Kakwale, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Januari 10, mwaka huu, wakiwa kazini kwa kutumia kofia ya askari polisi kuwaibia wananchi.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ally Hashimu (29) na Fitna Ramadhani (26), wote wakazi wa Temeke Mikoroshini.

"Habari za askari hao feki zilitufikia wakati na wao wakiwa na watu waliowakamata wakitumia sifa hiyo ya polisi ili kutimiza lengo lao la kuwaibia, kwa hiyo tuliwakuta wakifanya uhalifu, na baada ya kuwahoji walisema walikuwa wanatumia lugha ya kilaghai ili kujipatia kipato hicho haramu kupitia Jeshi la Polisi," alisema Kamanda Kakwale.

"Watu hao wamekuwa wakitumia vitambulisho bandia kwamba wao ni maofisa wa Jeshi la Polisi na wamekuwa wakiwaibia wananchi kwa vitisho na visingizio mbalimbali."

**WENYEWE WAZUNGUMZA**

Wakizunguma mbele ya waandishi wa habari watuhumiwa hao walisema, walikuwa watatu wakati wanatekeleza uhalifu huo, lakini mwenzao mmoja alifanikiwa kukimbia.

"Januari 8, mwaka huu, tulitoka nyumbani tukaja huku Kigamboni tukiwa watatu, tukawa tunachukua baadhi ya vitu kwa wananchi, lakini askari walivyotokea ili watukamate, mwenzetu mmoja alifanikiwa kukimbia," alisema mmoja wa watuhumiwa hao, Ally Hashimu.

Pia Kamanda Kakwale alisema katika tukio jingine maeneo ya Mbagala Mchikichini, katika wilaya hiyo ya Temeke walimkamata, Hassan Fahame, anayetuhumiwa kufanya vitendo vya wizi na ujambazi.

Alisema mtuhumiwa huyo wa ujambazi baada ya kupekuliwa alikutwa na vitu mbalimbali.

"Huyu tulimkamata kwa kuongozwa na simu ya kisasa hadi kwake na aliposikia askari wanabisha hodi alihamaki na kutoka na kisu akitaka kuwachoma, lakini waliwahi na kumpiga risasi katika maungio ya miguu," alisema.

"Alipopekuliwa nyumbani kwake kulipatikana simu saba za aina mbalimbali, vocha 147 za simu za kampuni tofauti, laini 10 za simu tofauti, visu viwili, tochi moja, plaizi moja, redio mbili, mabegi mawili ya mgongoni, mikoba saba ya kinamama, waleti mbili na headphone moja."

"Hivi vyote vilipatikana kwenye chumba chake na tayari wananchi wameshafika na kutambua mali zao."

Kamanda Kakwale alisema, jeshi hilo linaendelea kuwatafuta washirika wengine ambao walikuwa katika kundi moja la uhalifu huo na endapo watakamatwa wataunganishwa na wenzao hao na kufikishwa mbele ya sheria.

# Mlinzi mbaroni tuhuma mauaji ya mke

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linamshikilia mfanyakazi wa kampuni ya ulinzi ya Komesha, Shabani Mpacha, kwa tuhuma za kumuua mke wake kwa madai ya wivu wa kimapenzi.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana kwamba mtuhumiwa anadaiwa kumuua mke wake, Zainabu Yassin (46) wakiwa nyumbani kwao baada ya kutokea kutoelewana na kutokea ugomvi kati yao.

Inadaiwa kwamba Yasini alikuwa mke wa ndoa, lakini kwa muda mrefu alikuwa anatuhumiwa na mumewe kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamume mwingine, hali iliyosababisha kuwapo kwa ugomvi kati yao.

Bakari Yasini na Bakari Issa, ambao ni kaka wa marehemu, kwa nyakati tofauti walithibitisha kuwapo kwa ugomvi huo ambao chanzo chake kinadaiwa ni mtuhumiwa huyo kumkataa mtoto kwa madai kuwa hafanani naye hata kwa sura wala rangi.

Walidai kuwa kabla ya tukio hilo, dada yao alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru kwa ajili ya kumuuguza mtoto wake huyo wa miaka miwili aliyetajwa kwa jina la Miraco Shaibu.

Kwa mujibu wa ndugu hao, wakiwa nyumbani, mtuhumiwa alimwomba mkewe amwandalie chakula, lakini alikataa kwa madai kwamba mpaka amalize kumpatia dawa mtoto.

Walidai kuwa baada ya hatua hiyo, mtuhumiwa alimvamia mke wake na kumnyang'anya mtoto akidai kutaka kumuua ili kumfanya mkewe kuacha visingizio vya kushindwa kutoa huduma kwake kisa mtoto huyo ambaye alisema si damu yake. Hali hiyo, walidai kuwa ilimfanya Yasini kuanza kunyang'anyana mtoto huyo na kusababisha kuangushana chini.

Kutokana na valangati hilo, Yasini aliumia sana kichwani upande wa kisogoni, hali iliyowafanya majirani waliojitokeza kuamulia ugomvi huo, kumpeleka hospitalini lakini alifariki dunia wakiwa njiani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba polisi wanamshikilia mtuhumiwa na kwamba wanaendelea na uchunguzi. Maigwa pia alisema baada ya kukamilika kwa uchunguzi, mtuhumiwa atapelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Naye mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Dk. Stephen Hokororo, alisema chanzo cha kifo hicho ni kutokana na marehemu kutokwa na damu nyingi kichwani.

# Jafo awaweka kikaangoni wakurugenzi h/mashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKURUGENZI wa halmashauri tano zilizofanya vibaya kwenye utekelezaji wa mkataba wa lishe, wametakiwa kujieleza kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), sababu za kusuasua utekeleza wa agizo la ofisi hiyo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Selemani Jafo, alipokuwa akifungua mkutano wa tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe nchini kwa mwaka wa fedha 2019/20, jijini hapa.

Aliwataja wakurugenzi hao kuwa ni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Manispaa ya Bukoba, Misenyi, Masasi na Biharamulo.

"Katika tathmini iliyopita ya mikataba ya lishe, halmashauri 25 zilionekana kufanya vibaya kwenye utoaji wa fedha za lishe na tuliwataka wakurugenzi wajieleze, halmashauri zote zimefanya vizuri isipokuwa tano zimeendelea kusuasua katika kutekeleza maagizo yaliyotolewa na hili nawataka wakurugenzi hao waende kumuona Katibu Mkuu waeleze kwanini hawakutekeleza maelekezo yaliyotolewa na TAMISEMI," alisema.

"Mkurugenzi wa Halmashauri ya Biharamulo yeye kutokana na kuwa mpya anapaswa kueleza mikakati yake atakavyofanya ili kufanya vizuri kwenye masuala ya lishe."

Alisema utekelezaji wa masuala ya lishe kwenye maeneo mbalimbali nchini unaridhisha.

"Katika tathmini yetu ya mwaka 2019 tulielekezana kufanya tathmini kila baada ya miezi sita, niwapongeze mikoa yote japokuwa mikoa miwili haikufanya vizuri, Mkoa wa Kilimanjaro na Tabora ni imani yangu kupitia mkutano huu wa leo iwe ni fundisho kwenye eneo hili," alisema.

Aliitaka mikoa hiyo mwaka huu kufanya tathmini kama ilivyoelekezwa kwenye maazimio ya Agosti, 2019.

"Tuendelee kufanya juhudi za hali na mali kuhakikisha shughuli za lishe lazima tusimamie kwa karibu, lazima tuwe na mikakati endelevu ya masuala ya lishe, kuna maeneo hatufanyi vizuri kuna maeneo mradi wa lishe unapotekelezwa na kukoma utekelezaji wake watu tunajisahau kwenye utekelezaji sio jambo jema," alisema.

Alitoa mfano wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwamo Geita na Mwanza, baada ya mradi wa masuala ya lishe utekelezaji wake kukoma, ilionekana hali ya lishe imeshuka.

Waziri Jafo alisema Makamu wa Rais aliagiza kuwapo na mikataba ya utekelezaji na usimamizi shughuli za lishe mikoani.

Kuhusu Mkoa wa Rukwa, Jafo, alisema ni miongoni mwa mikoa mitatu nchini inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula, lakini tatizo la lishe limeendelea kuutesa na kuwataka viongozi wake watoe kipaumbele kwenye masuala ya lishe.

Awali, Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Ofisi hiyo, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema malengo ya mkutano huo kuweka mikakati ili kuchunguza vikwazo vya lishe kwenye mikoa isiyofanya vizuri licha ya kuwa na uzalishaji mzuri wa chakula.

Agosti, 2017, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliagiza kuwapo kwa mkataba wa utendaji na wakuu wa mikoa yote ya Tanzania Bara ili wasimamie utekelezaji wa shughuli za lishe katika mikoa yao ili kuondoa tatizo la utapiamlo nchini.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

## DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014

### CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:
a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.
b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

**Note:**
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**

a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)**

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**

The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk

## DISCLOSURE UNDER REGULATION 11 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES/FEES/PRODUCTS AND SERVICES

| | TZS | USD | D. REMITTANCES | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A. SAVINGS BANK | | | | TZS | USD |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 2. E Remittances | | |
| 3. A/C Statement Charges | | | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| a) Monthly | FREE | FREE | 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 | 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free Above 5000 - 0.3% | 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE | 3. SWIFT | | |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 | a) Swift Outward | | |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 | Upto 5,000 | NA | $45 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 | 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| B. CURRENT ACCOUNT | | | above 10,000 | NA | $90 |
| | | | b) Swift Inward | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE | Upto 5,000 | NA | $12 |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE | 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly b) Interm | **5000** **5000+500 for each page** | **$5** **$ 5+1 for each page** | above 10,000 | NA | $30 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free 5000 to 10,000 - 0.3% Above 10,000 - 0.5% | E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES | | |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE ABOVE 50 MIO--0.12% | **Upto 10,000- Free > 10,000- 0.3%** | 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000 5Mio to 10 Mio - 200,000 10 Mio to 25mio - 400,000 25 mn to 500 mio - 1.5% >500mio--1.25%* *minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500,000--1.25%* *minimum 7,500 |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 | 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL-- >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 | 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000 5 Mio to 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Upto 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *minimum 9000 |
| 7. Cheque Return Charges | | | 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25 >50,000 ----50 |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 | F. LETTER OF CREDIT | | |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 | Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 | Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |

| C. MOBILE BANKING CHARGES | | | LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Cash Withdrawal | | | Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA | Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA | Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA | LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA | Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA | Export Letters of Credit (per quarter or part thereof) | | |
| 2. Funds Transfer/Mobile Wallet | | | Advising commission | NA | $140 |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA | Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA | Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA | Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA | Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA | Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| | | | Amendments | NA | $75 |
| Mobile Banking Services | | | G. Guarantees (Local & International) | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA | Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |
| H. LOCKERS RENT YEARLY | | | | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | | | | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | | | | |
| 3. BIG | 750,000.00 | | | | |

OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 10 Million | Over TZS 10 Million up to 100 Million | Over TZS 100 Million up to 300 Million | Above 300 Million |
|---|---|---|---|---|
| 31 -90days | 3.00% | 4.00% | 5.00% | 4.75% |
| 91-180days | 4.00% | 5.00% | 6.00% | 5.75% |
| 181-364 days | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 6.75% |
| 1 Year and above | 6.00% | 7.00% | 8.00% | 7.75% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 5000 | Over USD 5000 up to 50,000 | Over USD 50,000 up to 100,000 | Above USD 100,000 |
|---|---|---|---|---|
| 31 -90days | 0.75% | 1.25% | 1.50% | 2.00% |
| 91-180days | 1.00% | 2.00% | 2.25% | 2.75% |
| 181-364 days | 2.25% | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| 1 Year and above | 3.00% | 3.50% | 3.75% | 4.00% |

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd** **We offer following Services**

- Current and Saving Account
- Salary Account
- Student Account
- Fixed Deposit Account
- Re Investment Deposit Account
- Recurring Deposit Account
- Overdraft and Term Loans
- Vehicle Loan
- Mortgage Loan
- Personal Loan
- Insurance Premium Funding
- Safe Deposit Lockers
- All Export and Import Related transactions
- Letter of Credit and Guarantees
- E- Remit Facility to India
- Mobile Banking



Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O.Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D)+255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

Access your A/c 24x7

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wajasiriamali wanatukera vituo vya daladala, mabasi

**VITUO** vya daladala kwenye maeneo mengi ya Dar es Salaam na miji mikubwa vimekuwa kero kwa abiria wawe wasafiri wanaokwenda mikoani au wanaotumia usafiri wa ndani kutokana na kuvamiwa na wajasiriamali wasiodhibitiwa.

Ni kero kwa maana sehemu hizo hazitumiki tena kwa malengo yaliyokusudiwa tangu mwanzo zilikuwa zimewekwa maalum kwa ajili ya abiria kupumzika ili kusubiri gari, kujikinga na mvua, jua au hata kuwa salama wakati mabasi yanapoingia vituoni.

'Stendi' hizo kama zilivyozoeleka kuitwa, leo zimegeuzwa kuwa maeneo ya biashara na wajasiriamali wamepata sehemu za 'kujiachia'.

Kwenye kiti (wanapokaa abiria) kumejaa uchafu kama mafuta yaliyokaangia vyakula kama mihogo, sambusa za viazi na pia njiti za mishikaki, kuna maganda ya miwa, machungwa na ndizi.

Lakini, pia stendi nyingine zimekuwa meza za kuwekea bidhaa mfano mabeseni ya matunda na nyungo zenye pipi, sigara, bisi, tambi, karanga na ndoo ambazo ndani yake kuna vitafunwa na vyakula mbalimbali.

Wakati wa mvua na jua kali, abiria hawana pa kusimama kujikinga kutokana na maeneo hayo kujaa wajasiriamali wanaouza bidhaa kwenye vituo vya mabasi.

Wapo wanaosimama na mizigo kichwani, wakijaa kila mahali mbele na nyuma na kuyafanya maeneo hayo kuwa kero kwani wasafiri hawana pakukimbilia kwa vile wafanyabiashara wamejipatia haki miliki ya sehemu hizo.

Tunajua kuwa viongozi wa miji na majiji si wageni, wanafahamu fika kuwa abiria wanaosimama vituoni ili kujikinga na jua kali la utosini au mvua wanakutana na meza zenye matunda, juisi, maji, biskuti, pipi na vitafunwa.

Ni dhahiri kuwa wauza bidhaa hao wanataka kupata wateja hivyo wanawazuia wasafiri kusimama mbele ya biashara zao kwa sababu wanawaziba wateja wasiwafikie.

Tunaona kuwa haipendezi ni kero kwa wasafiri wa miji na majiji mengi kuanzia Dar, Mwanza, Mbeya, Tanga na Arusha kwa vile wajasiriamali wamevamia vituo hivyo ambavyo vilikuwa vimewalenga wasafiri.

Pamoja na ukweli kuwa biashara inahitaji kufanyika kwenye mkusanyiko mkubwa wa wateja wakiwamo wa vituo vya abiria ni wakati wa kuandaa utaratibu wa kuzuia wavamizi kwenye sehemu hizi.

Imekuwa ni kero ya muda mrefu ambayo manispaa na majiji yanatakiwa yaanze kuchukua hatua kuzimaliza na kurejesha hadhi kwenye sehemu hizo.

Ni wazi kuwa wafanyabiashara hawa wanavamia vituo baada ya kujaza bidhaa zao kwenye njia za wanaotembea ambazo zilikuwa maalumu kwa wasiotumia vyombo vya moto.

Sehemu hizo zimepangwa biashara au bidhaa mbalimbali kama viatu, nguo, matunda, pweza, ngisi na samaki wabichi na chips pamoja na mishikaki vyote hivyo vikiwapa shida wanaotembea. Tunazikumbusha mamlaka kuwa si jambo jema kuendesha mambo bila utaratibu wa kisheria.


Kama njia zilizowekwa kwa ajili ya wanaotembea zimepangwa bidhaa inamaanisha kuwa wahusika hao wanalazimika kuingia barabarani kupambana na magari, bodaboda na bajaji matokeo yake ni kuhatarisha maisha yao na ajali.

Tunawakumbusha wasimamizi wa maeneo haya ambao ni halmashauri za wilaya na manispaa za miji na majiji, maofisa, kamati za mazingira na usafi kufuatilia kuondoa kasoro hizo, kuandaa sheria za kudhibiti na kutoa elimu ya matumizi ya maeneo mbalimbali kwenye miji na majiji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera ofisi kijiji kufanikisha maendeleo kwa wakazi staili hii

Na Yasmine Protace, MKURANGA

**OFISI** za vijiji zina wajibu wa kutumia fursa walizo nazo katika vijiji ili kutatua changamoto katika maeneo yao.

Hapo kuna wawekezaji wanakuja kuwekeza na hao wakitumiwa vizuri wanaleta maendeleo makubwa katika maeneo yao.

Kama ofisi za vijiji vitajikita kusimamia vizuri vyanzo vya vyake vya mapato, ni haki inayokifanya hata kijiji kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Uzoefu unaionyesha kuna baadhi ya vijiji havina maendeleo, lakini ukiangalia upande wa pili wa shilingi, ni mahali panapofanyika uwekezaji mkubwa.

Hapo ndipo penye hatua inayozaa swali, inakuwaje kijiji kilichobeba sifa kamili kinakosa sura na mwonekano wa kukosekana maendeleo, wakati kuna wawekezaji wa kutosheleza mahitaji.

Kinachotakiwa hapa ni viongozi husika wa vijiji kukaa pamoja na kushirikiana na wawekezaji, ili kuhakikisha maeneo yenu sahihi yanasonga mbele katika tija ya maisha.

Tunafahamu kuwa daima wawekezaji kabla ya kuingiza mitaji yao katika sehemu zetu, wanakubaliana na kijiji kuhusu vitu vya kimaendeleo, ambavyo watakifanya kwa faida ya wanakijiji.

Pia hata ofisi ya kijiji inaweza kutumika rasilimali za kijiji kwa ajili ya kutatua kero za wananchi na sio kila kero ikatatuliwe na serikali. Hapana! Lazima kuwa na mikono yetu walau kwa asilimia fulani.

| | - Individual | USD 3.00 (USD a/c) TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |
| | - Corporate | USD 10.00 (USD a/c) TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | | TSHS |
|---|---|---|---|---|
| e) | Others | - | | - |
| 5.0 | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |
| 6.0 | **Other Charges** | | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per | | | |
| | - Individuals | 3 | | 5,000 |
| | - Corporate | 6 | | 12,000 |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 7.0 | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| 8.0 | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| 9.0 | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| 10.0 | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 07.01. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 07.01. 2021 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 07.01. 2021 |

### OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 4.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 5.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 6.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 7.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 7.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 8.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 0 7.01. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 0 7.01. 2021 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 0 7.01. 2021 |



Ukurasa 12

## Kuyumba soko la nyanya kuvuka mpaka kunavyowaacha taabani wauzaji Tarime


BUFE

IJUMAA JANUARI 15, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

## MGOGORO MPAKA ZAMA 1952...

### Waziri azuru hifadhini Kilombero akimaliza msuguano na wananchi

# DED Mkuranga ajinasibu na stendi Sh. bil. 50, mwendokasi ina egesho

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

MKURANGA nako sasa kumekucha. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo mkoani Pwani, Mhandisi Mshamu Munde, anasema wako mbioni kujenga stendi ya kisasa katika eneo la Mwandege.

Hapo lengo kubwa ni kuhakikisha wananchi wanufaika na fursa zinazowazunguka katika mtazamo wa usafiri.

Anasema katika kufanya hilo fursa anazotaja zitakuwa katika stendi hiyo na itakuwa pia ni mpango wa uchumi kwa Mkuranga, huku akifafanua kwamba ni stendi inayolenga kuhudumia, pia mabasi yaendayo mikoa ya Kusini na nchi jirani.

Mkuranga iko katika bararabara kuu inayounganisha Jiji la Dar es Salaam, inayopakana na mikoa ya Kusini Lindi, Mtwara na Wilaya ya Tunduru mkaoni Ruvuma, pia nchi jirani ya Msumbiji.

Anasema, kukamilika kwa stendi hiyo kutawaondolea abiria kero ya usafiri wanayokutana nayo, Mbagala jijini Dar es Salaam, ikiwa stendi yenye ukubwa wa ekari 50.

"Hii stendi itakuwa kubwa na ya kisasa na itatoa huduma za maegesho ya malori, mabasi makubwa, mabasi madogo magari ya watu binafsi na mabasi ya mwendokasi," anasema.

Anafafanua wameishaongea na wakala mabasi ya mwendokasi, ambako mabasi hayo yatawachukua abiria kutoka nchi jirani na wale wa nchini.

Mhandsi Munde anaeleza matarajio ni kwamba, stendi ijayo itakuwa ya kisasa yenye maeneo yaliyotengwa kwa biashara za kada mbalimbali, akitaja mojawapo ni fursa kwa Machinga.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo mkoani Pwani, Mhandisi Mshamu Munde. **PICHA: YASMIN PROTACE.**

Aidha, anasema kutakuwapo maeneo ya bustani ya bustani za mapumziko na kufanyia faragha mbalimbali, kama vile kutumia kupiga picha na hata kutumiwa na wanaorekodi nyimbo.

Mkurugenzi Mtendaji anautaja kuwa ni mradi mkubwa utakaokuwa na huduma mbalimbali za kijamii kwa utaratibu maalum kwa wahitaji.

Anaongeza kuwa mpaka sasa, wapo katika hatua za usanifu na hadi mwisho wa mwezi huu, watakuwa wanafanya uchambuzi na kufautiwa na hatua ya kuandaliwa ramani.

"Ramani zitapelekwa katika taasisi za kuombea fedha, lakini sio benki," anataja chanzo cha uwezeshaji mradi, akifafanua kuwa itafuatiwa na

dokezo kupelekwa Ofisi ya Hazina, kuomba fedha za kufadhili mradi, unaotarajiwa kugharamu fedha Sh. bilioni 50.

Anasema halmashauri yao inatarajia kuanza katika mpango kazi wa fedha kidogo kujenga mahitaji kidogo yaliyo muhimu, ili mradi uanze kutumika wakati sehemu nyingine ya ujenzi ikiendelea.

Anafafanua:"Tutaanza na kiasi hicho cha fedha, tutazalisha na kujihudumia sisi wenyewe, ili tuimalizie miundombinu ambayo itakuwa haikukamilika."

Dk. Festo John Dudange, kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI) Kitengo cha Afya, Mapato na Miundombinu, akiwa ziara ya siku moja katika wilaya hapa, anaipongeza Halmashauri ya Mkuranga kwa jitihada hizo za kimaendeleo kujenga stendi ya kisasa.

Anasema, kuanzishwa stendi kutawasaidia kuinuka kiuchumi zaidi, pia wana - Mkuranga watapata ajira itakayochangia kubadilisha maisha yao.

Dk. Festo, anazikumbusha wilaya zote nchini kupanga mikakati ya ukusanyaji mapato ya ndani, ili yafikie asilimia 50 ya malengo watakayofanikisha kuwatatulia wananchi magumu katika sekta zao mbalimbali.

Kuhusu miradi ya barabara, anasema mingi inashindikana kuendelea, kutokana na kutotekelezwa kwa mikataba ya barabara, kwani wajenzi wengi hawakidhi vigezo.

Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega, anasema makandarasi wengi wanaoletwa kufanya kazi vijijini, hawana uwezo na wanasababisha kazi kukwama na anatoa mfano kuwapo wanaofanya kazi kwa dai kwanza la kupatiwa fedha.

"Inatakiwa makandarasi wafanye kazi, pesa italipwa, lakini baadhi yao wanatanguliza pesa," anasema Ulega.

Mkuu wa Wilaya Mkuranga, Filbeto Sanga, anasema miundombinu ya barabara ina changamoto anauomba Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), uongezewe uwezo.

Anafafanua uwiano wa mgao wa fedha za makusanyo kuwa, asilimia 30, zinachukiwa na TARURA na asilimia 70 kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD).

Sanga anaendelea: "TARURA iongezewe bajeti ili iweze kwenda sambamba na kutoa huduma katika barabara za vijijini na madaraja."

BIASHARA

# Kuyumba soko la nyanya kuvuka mpaka kunavyowaacha taabani wauzaji Tarime

## • Simulizi za Mwanamke Jasiri, Bibi Hellena

**Na Anthony Gervas, aliyekuwa TARIME**

WILAYA ya Tarime, nyanya iko katika mazao yake yanayolimwa kwa wingi. Soko lake kubwa kwa muda mrefu lilitegemea ndani na kuvushwa mpaka wa nchi jirani, ambako kwa sasa mambo hayako sawa.

Baada ya kuingia ugonjwa wa corona na kufungwa mipaka, biashara hiyo imedoda na kubaki soko la walaji na wanunuzi wa ndani, hali inayowafanya wafanyabiashara wadogo hivi sasa wanakiri kushuka bei ya mauzo.

Vilevile wafanyabiashara hao waliokuwa wakiuza katika soko kuu la mjini Tarime na baadaye kuhamishiwa katika soko la muda la Rebu mjini humo kupisha ujenzi wa soko kuu la kisasa, nalo ni pigo kwao.

Makamu Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wadogo katika Soko la Rebu, Daniel Maghabe, anaelezea magumu yanayowakabili kuwa ni pamoja na kushuka bei ya nyanya katika soko hilo.

"Ugonjwa wa corona na kubomolewa soko, kumechangia kuzorotesha bei ya zao hilo na kuleta kilio kwa wafanyabiashara wadogo mjini Tarime, ikiwa tenga kubwa la ndoo sita za lita 20 tunauza Sh.35,000 hadi Sh. 45,000, badala ya Sh. 50,000 hadi Sh. 70,000 ilivyokuwa awali," anasema.

Maghabe anaeleza kuwapo wafanyabiashara ambao mitaji yao imekatika, baada ya kuhamishiwa katika soko hilo kupisha ujenzi, wakiwa katika hatua ya kulazimika kuacha biashara hiyo.

Anasema, tegemeo la soko hivi sasa limehamia kwa walaji wa rejareja, kuliko wa jumla waliotegemewa zaidi mwanzoni, kabla ya bei kushuka.

Mwenyekiti huyo anajigamba kuwa wilayani Tarime ni kitovu kikubwa cha mazao ya biashara kama vile ndizi, nyanya na mahindi, kilimo kikiwa ni cha mwaka mzima pasipo msimu wa kiangazi wala masika, kutokana na hali ya hewa iliyopo.

Anaiomba serikali iwaharakishie ujenzi wa soko jipya la kisasa, akiamini litawaokoa wafanyabiashara wadogo waliohamishwa kutoka mtihani wa biashara kuwa mbaya zaidi mahali wanakopatikana.

"Serikali iharakishe ujenzi wa soko la kisasa ili wafanyabiashara hawa warudi kule mjini kati, kwa sababu kwanza huku hakuna vibanda rasmi vya kuuzia na wanauzia eneo la wazi, wananyeshewa mvua na jua pia ni lao," anasema Maghabe.



Prisca Samson maarufu Bibi Jasiri, akiwa kwenye biashara yake ya kuuza nyanya katika soko la Rebu, mjini Tarime.

> **"Mimi siwezi kubadilisha biashara nyingine tofauti na nyanya, hii nimeshaizoea pamoja na kwamba sasa hivi hali ya biashara ni ngumu, wengi wamekatika mitaji na kulazimika kuiacha baada ya kuhamishiwa kwenye soko hili la Rebu, lakini mimi naendelea kupambana," anasema.**

**MWANAMKE JASIRI**

Prisca Samson, ni mwanamke aliyejitambulisha kuwa 'jasiri wa biashara ya nyanya' aliyeifanya miaka mitano sasa. Anasema, pamoja na misukosuko ya soko, msimamo wake hawezi kuiacha au kuhamia biashara nyingine.

Sababu yake kuu ni kwamba ameshaizoea na kumudu misukosuko, hata kama wengine wemeweza kufilisika mitaji yao na kuiacha.

"Mimi siwezi kubadilisha biashara nyingine tofauti na nyanya, hii nimeshaizoea pamoja na kwamba sasa hivi hali ya biashara ni ngumu, wengi wamekatika mitaji na kulazimika kuiacha baada ya kuhamishiwa kwenye soko hili la Rebu, lakini mimi naendelea kupambana," anasema.

Prisca anasema kuwa, wakati anaanza biashara hiyo katika soko kuu la zamani, alikuwa na mtaji wa Sh. 200,000, lakini baada ya kuhamishiwa soko la muda Rebu, aliongeza mtaji wake na kufikia Sh. 500,000 ili kuongeza kipato chake cha kila siku.



Makamu Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wadogo wa Soko la Rebu mjini Tarime, mkoani Mara, Daniel Maghabe, akiwa katika mauzo ya nyanya.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Ntiruhungwa.
**PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

Mwanamke jasiri, ana ufafanuzi wa kilio kikubwa walicho nacho cha kuoza kila siku, hivyo inawasababisha wengi 'kukatika' mitaji yao na kushindwa kuimudu biashara hiyo.

"Mimi naiomba Halmashari ya Mji wa Tarime, itoe ushirikiano kwetu wafanyabiashara wadogo kutujengea kiwanda kidogo cha kusindika nyanya, ili kuboresha biashara zetu ambazo tutauza kupitia vifungashio maalum," anasema Prisca.

Pia, anasisitiza pindi kukijengwa kiwanda hicho, anatazamia biashara itakuwa ya kisasa na inayoenda na wakati, hata kuwaepusha na shida ya nyanya kuoza, jambo linalowaacha kwenye hasara kubwa, ikiwamo akiitacho 'kukatika mitaji.'

Rai yake ni kwamba, hadi sasa wao wajasiriamali wa nyanya wako tayari kuanzisha kikundi cha kuchangia ujenzi wa kiwanda kidogo, endapo halmashauri ya mji huo, itawasikiliza kilio kuhusu adha hiyo tajwa inayowakabili kupitia biashara hiyo.

Je, ataiacha? Prisca anaweka bayana yuko kinyume na mwelekeo huo, kwamba ataendelea kuvumilia msikosuko katika safari hiyo ya ujasiriamali wa nyanya na kidogo anachokipata, kina maana kwake na familia inayoundwa na mume na watoto wanane.

Anasema, matarajio aliyonayo ni kwamba, kujengwa kiwanda cha kusindika mazao, kutabadilisha maisha yao kiuchumi na hata kuwarejesha wenzao katika biashara waliokata tamaa kutokana na kukatika mitaji, vivyo hivyo kwa waliobadilisha aina ya biashara, warejee walikotoka.

Prisca anaeleza kwamba, kwa soko lililopo limewaathiri mno, akitoa sababu kwamba biashara ya sasa inasuasua, hata wanapaza sauti serikali iharakishe mradi wa ujenzi wa soko jipya, kwani wateja walio nao ni wachache, kulinganisha na zamani.

Pia, mama huyo anautaja ugonjwa corona umechangia kuyumbisha kibiashara yao, hivyo wanunuzi wa nyanya kutoka nchi jirani Kenya waliokuwa wakinunua katika soko la mpakani Sirari hawakutokana tena hivi sasa, hali inayozipa pigo la soko kwao.

**BIBI MUUZA NYANYA**

Helena Charwi, ni bibi mwenye umri zaidi ya miaka 65 mfanyabiashara wa nyanya katika Soko la Rebu, anasema amevumilia mengi, kwani anauzia kwenye eneo la wazi lisilokuwa na kivuli, hivyo jua na mvua anavitambulisha vyote vyake.

"Kama unavyoona hakuna kibanda, meza, wala kivuli. Natumia mwamvuli kukaa hapa juani, ila mvua ikija naenda kujikinga baadaye ikikatika narudi kuendelea na biashara yangu, ili nipate riziki," analalamika.

Bibi Helena anasema, anauza nyanya na hawezi kuhamia mbadala kama shambani, kikuu kwake anachofafanua ni "ili mradi mkono unakwenda kinywani," kwa maana anachouza kila siku ndiyo kinampa riziki ya kuvuisha jua hadi kiza.

Anasema, kuna siku za 'mafuriko ya nyanya' na wakati zinaadimka, lakini hizo zote zinasimama katika usawa wa bei ya kundi kwa maana ya kutopishana sana, wakiwa wavumilivu wasiokata tamaa.

Kwa mujibu wea Bibi Helena, huwa anauza nyanya zake kwa bei za rejareja, fungu moja lenye nyanya sita Sh. 500, na zingine zina nyanya tano, pia nne kwa bei ya za walaji wa kawaida.

Soko kuu la zamani mjini Tarime lilibomolewa mwaka juzi kupisha ujenzi wa jipya la kisasa, ambao hadi sasa haujaanza kufanyika, hali iliyochangia kuyumba kwa biashara na soko la nyanya.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Waziri fikiria TV na magazeti haya





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

BISMILLAHI! Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, kwa kutotaka kujifanya nguli na badala yake kuamua kuwazungukia na kuwaita wadau wa tasnia ya habari, kujifunza kwao.

Amefanya hivyo, kwa kueleza akijuacho na kusikiliza asichokijua na hatimaye kuungana na wadau, kwa maana ya waandishi, wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari, kuamua mustakabali wa tasnia hiyo nchini.

Mbali na kusikiliza matatizo yanayoikabili tasnia hiyo pamoja na fursa zilizomo, waziri kwa niaba ya serikali, aliahidi kushughulikia mambo hasi yanayovikabili vyombo mbalimbali ambavyo vimekumbwa na adhabu, kutokana na mwenendo uliobainika kwenda kinyume na sheria, maadili au kanuni za uendeshaji wao.

Suala kubwa lililojitokeza katika majadiliano na baadhi ya wadau, ni la kituo cha habari cha Wasafi Media, ambacho televisheni yake imefungiwa kwa miezi sita, kutokana na ukiukaji maadili, uliofanywa na msanii wa kizazi kipya maarufu kama Giggy Money.

Waziri katika hilo, aliahidi kuanza nalo na kuona jinsi hatua hiyo ya kifungo itakavyoshughulikiwa na ikiwezekana kutafuta unafuu. Hilo ni jambo la neema si kwa kituo hicho tu, bali pia kwa wateja wake yaani watazamaji.

Hapo, waziri kaingia kama mzazi au mlezi wa vyombo vilivyo chini yake, kwa kutafakari na kubaini athari hasi zinazojitokeza kwa wadau wa fani hiyo na televisheni kwa ujumla.

Lakini wakati akifanya hivyo, ni bora akautumia pia uzazi na ulezi huo, kuitisha majalada yanayohusu vyombo vingine vilivyokumbwa na kadhia hiyo, na kuona jinsi ya kuvifikiria, ikiwezekana kuvisamehe au kuviruhusu virejee mitaani na wadau wao wapate ahueni.

Vyombo hivyo ni pamoja na magazeti ya Mwanahalisi, Mawio, Mseto na Tanzania Daima; lakini Kwanza TV. Najua, waziri anajua kuwa katika maisha kuna kukosea, pia kuna adhabu inayofuata na lazima viendane, ingawa anajua pia kuwa kuna kusameheana, hasa baada ya mkosaji kuomba radhi na kuonyesha kujirudi.

Ndiyo sababu hata katika mashtaka mengine yanayofuatiwa na adhabu za vifungo serikalini, huwa kuna Kamati ya Parole ambayo huishauri serikali kutoa msamaha kwa wafungwa walioonyesha kujirudi na kujirekebisha.

Wizara ya Habari haina Kamati ya Parole, lakini ina watu wanaomshauri waziri na kufuatilia adhabu na mabadiliko kwa mkosaji na kuamua kumpa nafuu, ili aweze kuendesha maisha yake, huku wadau wake nao wakiendelea kupata huduma.

Kwa kuwa Waziri Bashungwa ameonekana kuwa msikilizaji na msikivu, ni matumaini yangu kuwa ushauri huu atauzingatia, ataita wahusika na kuzungumza nao au hata bila kuzungumza nao, ataangalia upya adhabu zao na kuziondoa kama si kuzipunguza, lakini akiwataka kufuata maadili yaliyopo.

Kufungia chombo cha habari kwa sababu yoyote ile, kunafinya fursa ya wananchi kupata habari wanazohitaji, ingawa hiyo pia si fursa kwa vyombo kuandika au kurusha chochote bila kuzingatia maadili, kwa kuwa tu vinapata kipato au umaarufu.

Ni dhahiri hata sasa, kwamba adhabu hizo maumivu yao hayalingani kati ya chombo kimoja na kingine. Mathalan kufungiwa Wasafi TV athari yake hailingani na ya magazeti yaliyotajwa hapo juu.

Kwa nini? Wasafi TV imefungiwa, lakini Wasafi FM iko hewani na watangazaji ni wale wale, hivyo dhana kwamba kwa miezi sita hawatakuwa kazini huenda si halisi. Kufungiwa kwa magazeti hakuna mbadala, waandishi karibu wote watakuwa nje ya kazi mpaka adhabu iishe.

Kufungiwa kwa Giggy Money kwa miezi sita ndani na nje ya nchi na kutozwa faini ya Sh. milioni moja, maumivu yake ni tofauti na ya Wasafi TV, kwani Giggy hataingiza chochote zaidi ya kutoa, huku kituo cha Wasafi kikiendelea kuingiza kupitia matangazo ya biashara.

Niwashauri au kuwahadharisha watangazaji wetu wa kizazi hiki katika vituo vya redio na televisheni, kujitahidi kufunga gavana kwenye ndimi zao, kwani ndizo zimekuwa zikiponza vichwa vyao, kwa kukiuka maadili ya utangazaji. Alamsiki!

UCHUMI

MGOGORO MPAKA TANGU ZAMA 1952...

# Waziri azuru hifadhini Kilombero akimaliza msuguano na wananchi

- Asema wameshtukia hujuma za hifadhini
- Ruksa vijiji 41, 'vigezo na masharti' vyaja
- Mbunge apiga debe uvuvi, nako akubaliwa

**Na Christina Haule, KILOMBERO**

SERIKALI imeamua kumaliza mgogoro wa mipaka kwenye Bonde la Mto Kilombero uliodumu muda mrefu baina ya wananchi waliovamia Hifadhi na Mamlaka za Uhifadhi, huku mipaka hiyo ikiwa haina athari kwa wakazi wa vijiji 41 kati ya 42 vilivyopo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumaro, akiwa katika hadhara iliyowakusanya watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), anasema, wanavijiji 41 wataendelea kubaki kwenye bonde hilo, baada ya Rais John Magufuli kuwapa hisani hiyo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumaro, akiwa katika mkutano ndani ya Pori Tengefu la Kilombero wiki hii. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Anasema, hivi karibuni kamati ya mawaziri wanane itawaita wakuu wa mikoa yote jirani kuwapa maelekezo ya mipaka ya vijiji hivyo 41 na wananchi watakaokuwapo, watatakiwa kuondoka kwa hiari kwenye bonde hilo, kwa maslahi ya taifa.

Dk. Ndumbaro amewaambia wanavijiji hao watakaobaki wafuate sheria za utunzaji vyanzo vya maji, ikiwamo kuacha kulima hadi watakapopatiwa mkataba wa mipaka mipya na miongozo ya kisera inayosisitiza maeneo ya kuendelea kuhifadhiwa.

Waziri Dk. Ndumbaro, anawataka wakazi kutambua mipaka ya bonde hilo iliyowekwa mwaka 1952 pori lilipoanzishwa na mabadiliko yake ya mwaka 1997 na mkataba mpya unaofanyiwa mchakato sasa.

"Mipaka hiyo ya zamani ipo na ilitolewa ikiwa na matangazo ya serikali, haijawahi kubadilishwa," anasema.

Dk. Ndumbaro anasema, kinachoonekana kimatendo kwenye bonde hilo hadi kufikia uvamizi ni hujuma ya watu yenye athari kwa Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere, zikiwamo kuwapa wanavijiji mbegu za mazao zinazonyonya maji mengi, jambo ambalo serikali imegundua na kuchukua hatua stahiki.

"Mtu yeyote anayehujumu mradi wa Mwalimu Nyerere kwa maneno na matendo atafikishwa mahakamani kupata anachostahili.

"Uhujumu uchumi ni kama mtu hutaki mradi wa umeme ufanikiwe wewe ni mhujumu uchumi, rushwa ni matendo ya watumishi na watendaji wa hifadhi kujipatia rushwa.

"Utakatishaji fedha ni kuzibadilisha fedha zinazopatikana kwenye mfumo usio rasmi, kuwa kwenye mfumo rasmi na ujangili ni vitendo vya rushwa na kufanya 'sheshe', viboko na tembo kuendelea kupungua kwenye bonde," anasema Dk. Ndumbaro.

Anasema pori hilo tengefu linachangia asilimia 65 ya maji yote yanayoenda kwenye bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere.

### KUPANDA CHEO

Ni katika tukio hilo, Waziri Dk. Ndumbaro, amempandisha cheo Ofisa Mhifadhi Daraja la Pili, Laurent Juma Okode, kuwa Ofisa Mhifadhi Daraja la I, kutokana na uaminifu wake, akitekeleza majukumu ya ya kazi akiwa Meneja wa Pori Tengefu la Kilombero.

Ni tukio lililoendana na kuwavua vyeo na kuwafuta kazi watumishi watatu, kutokana na madai na tuhuma za rushwa, kujihusisha na ujangili na utakatishaji fedha.

Anasema, mapato ya sekta utalii yanachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa, huku ikiingiza robo (asilimia 25) ya fedha za kigeni na lengo ya wizara ni kuongeza mapato yake maradufu.

Dk. Ndumbaro anasema, uvamizi katika pori la hifadhi kuchangiwa na uvamizi wa maeneo unaoendekezwa na viongozi wakuu kwenye wilaya husika, wanaotoa vibali vya vijiji, bila tathmini ya kina eneo hilo ni la mahitaji gani.

Anawataka wakuu wa wilaya hao kuwa makini kabla ya kuanzisha kijiji kipya katika maeneo yao, kwani inaweza kusababisha wananchi kuingia na kuishi kwenye maeneo ya muhimu na vyanzo vya maji na hifadhi za serikali.

Ni ufafanuzi unaoangukia mfano wa Bonde la Mto Kilombero, eneo linalotarajiwa kuingia kwenye mkataba wa kimataifa uitwao RAMPSA.

Rai ya waziri kwa wahifadhi nchini ni kwamba, walinde maeneo yao kisheria na wasiruhusu watu kuingia na kuharibu, ikiwa sehemu ya kuungana na jitihada za serikali zinazoendelea katika sekta hizo, akiitaja kuwa ni njia mojawapo ya kuitii sheria bila shuruti.

Dk. Ndumbaro anatambulisha sehemu ya adhabu kwa wakosaji kwamba kila ng'ombe atakayekutwa kwenye bonde hilo atalipa faini ya Sh. 300,000 na mmiliki atalazimika kulipa fidia ya uharibifu alioufanya mnyama baada ya tathmini kufanyika.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, James Ihunyo, akiwa katika mkutano na wakazi, kujadili migogoro ndani ya Pori Tengefu la Kilombero, mwaka 2018. **PICHA: MTANDAO**

### UVUVI RUKSA

Pia anawataka wanavijiji watakaobakia ndani ya bonde hilo, kuendeleza shughuli kama za uvuvi, wakifuata taratibu zitakazowekwa na TAWA, baada ya mipaka mipya kuwekwa.

Anasema kwa sasa TAWA wanajipanga kutengeneza soko la samaki kwenye maeneo hayo, ikiwa ni utekelezaji wa ombi la Mbunge wa Jimbo hilo, Abubakar Asenga, alilolitoa mbele ya waziri.

Wzairi Ndumbaro anasema, baada ya kuwekwa mpaka mipya, bonde hilo litakuwa na sehemu maalum ya kuegesha mitumbwi na wavuvi watapata nafasi ya eneo la kuvua na kwenda eneo la mauzo.

"Tatizo la wavuvi wengi wana tabia ya kuvua samaki, kulima na kujenga kandokando ya mto bila kujali uhai wa mto huo. Hayo hayaruhusiwi tena," anasema Dk. Ndumbaro.

### NAIBU WAZIRI NA DC

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anasema bonde hilo limo katika orodha ya maeneo yenye hadhi kimataifa, kuwa na ardhi oevu yenye kilomita za mraba 6,500 na linalohitaji kutunzwa sana, pasipo uharibifu wa aina yoyote.

Anawataka wananchi kuona umuhimu wa kuzingatia sheria zilizopo, kwa kuacha kuvamia na kuishi kwenye maeneo ya mapito ya wanyama (shoroba), hali inayobabisha matukio ya vifo na vitisho kwao, kutoka kwa wanyama wakali, hali inayoongezeka kila siku.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, anaiomba wizara kutoa msimamo utakaozisaidia wilaya tatu za Ulanga, Kilombero na Malinyi, ukaoutumia kama dira ya kuendelea kusimamia bonde hilo.

Mlawa anasema, wamekuwa wakipigania kuhakikisha watu hawaingii ovyo kwenye bonde hilo na ututuzi wa migogoro hiyo ya muda mrefu, utakaosaidia kuzifanya wilaya hizo kuishi kwa amani.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzukwi, anawasisitizia wahifadhi waendelee kuzingatia kazi waliopewa kwa niaba ya Mungu.



# Usambazaji vifaa mahitaji maalum wazinduliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, amezindua usambazaji wa vifaa maalum vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa shule za msingi na sekondari vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.8.

Akizungumza jana jijini hapa katika uzinduzi huo, Jafo alisema hatua hiyo inalenga kutekeleza azma ya serikali ya kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeachwa nyuma, ambapo wanafunzi hao 18,488 watapatiwa vifaa hivyo.

"Lengo letu ni kuwapo na mazingira rafiki katika utoaji wa elimu. Tuna kila sababu ya kumshukuru Rais John Magufuli kwa uwekezaji kwenye elimu. Leo tunaanza na ugawaji wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao wamegawanyika katika makundi manane," alisema.

Jafo alisema vifaa hivyo vitasambazwa kwenye shule zote zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao kwa muda mrefu walikuwa wakikabiliwa na vikwazo katika kupata elimu.

"Wanafunzi wenye mahitaji maalum walikuwa wakifanya vibaya kwenye mitihani yao kutokana na kukosa vifaa saidizi. Sasa ni imani vifaa hivi vitafika kwenye makundi yote kama tulivyopanga, nafahamu vifaa hivi ni vya kisasa sana ni jukumu la walimu wetu kuhakikisha vifaa hivi walimu wanakuwa mstari wa mbele kuwasaidia wanafunzi kuvitumia vizuri," alisema Jafo.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa sera ya elimu na kwamba vifaa hivyo vitatumika katika makundi yote yenye ulemavu ikiwamo wanafunzi wenye ulemavu wa viungo, wasioona, viziwi, usonji, ulemavu wa ngozi, na wenye matatizo ya akili.

"Niwaombe vifaa hivi vitunzwe imani yetu vitawekwa kwenye mazingira bora ambayo itasaidia kutumika muda wote," alisema. Awali, Jafo alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imetoa Sh. trilioni 1.03 kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo na kwamba itaendelea kutekeleza mpango huo.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Joseph Nyamhanga, alisema serikali imekuwa ikinunua na kuwezesha vifaa vya kujifunzia na kufundishia elimu maalum.

Nyamhanga alisema kwa miaka mitano kumekuwapo na ongezeko la shule kwa ajili ya wanafunzi wa mahitaji maalum kwa asilimia 46.1 kwa shule za awali, asilimia 23.9 kwa shule za msingi na asilimia 24.6 kwa shule za sekondari.

"Uandikishaji wanafunzi wenye mahitaji maalum umeongezeka kwa asilimia 46.1 kwa shule za awali, asilimia 34 kwa shule za msingi na asilimia 74.6 kwa shule za sekondari na kuna walimu wa elimu maalum 418," alisema.

Nyamhanga alisema katika kipindi hicho pia Sh. bilioni 42.3 zimetumika kwa ajili ya chakula katika shule za msingi za bweni zinazohudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Alibainisha idadi ya wanafunzi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba kwenda sekondari imekuwa ikiongezeka kutoka wanafunzi 1,117 ambayo ni asilimia 69.9 kwa mwaka 2016 hadi kufikia wanafunzi 2,534 ambao ni asilimia 76.3 kwa mwaka 2020.



Mkazi wa Jiji la Dodoma (katikati), akichagua sare za shule kwa ajili ya mtoto wake, katika Mtaa wa Oneway, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watoa elimu kukabiliana na majanga

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limekubaliana na Chama cha Skauti kuanza kutoa elimu ya kuzuia majanga baada ya kubaini wanafunzi kusababisha hitilafu za umeme shuleni kutokana na vifaa wanavyotumia.

Akizungumza jana na Nipashe, Inspekta wa Jeshi hilo, Joseph Mwasabeja, alisema uchunguzi wao katika majanga ya moto yaliyotokea kwenye baadhi ya shule nchini wamebaini wanafunzi wanachaji simu kupitia nyaya zilizochunwa, kusahau kuzima pasi baada ya kunyoosha nguo na kusababisha hitilafu ya umeme.

Mwasabeja alisema anaamini skauti watashirikiana na jeshi hilo, kutoa elimu kwa wanafunzi na itasaidia kujikinga na majanga ya moto na mengine ambayo hutokea.

"Tumeamua kuingia makubaliano ya kuwapa mafunzo skauti ili kuwatumia kusaidia kwenda kutoa elimu hiyo katika maeneo ya shule na kwingineko," alisema.

Alisema utoaji elimu huo unatarajiwa kuanza hivi karibuni, ambapo mpango upo kwenye hatua za mwisho za kukamilishwa.

"Tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha vipengele ambavyo tutaenda kuwafundisha tutalenga zaidi utoaji elimu ya kujikinga na majanga ya moto na mengine," alisema Mwasabeja.

Alisema wameanzisha klabu za zimamoto katika shule za msingi na sekondari ambazo zitasaidia katika uelimishaji kwa wanafunzi juu ya namna ya kujikinga na majanga ya moto.

Alisema hadi sasa ziko klabu 786 katika mikoa yote hapa nchini ambazo wanachama wake wanaelewa masuala ya kujikinga na majanga ya moto na mengine.

Inspekta Mwasabeja alisema klabu hizo zimekuwa zikisaidia kuhamasisha wanafunzi wenzao kuhusu juu ya kujikinga na majanga hayo.

# Waomba utaratibu mafunzo ya kilimo, mifugo kwa vijana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo ya kilimo na ufugaji kwa wanafunzi wa vyuo, ili kuwaandaa kujiajiri wenyewe wanapohitimu masomo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Glaring Future Foundation (GFF), Mhandisi Aisha Msantu, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano uliowakutanisha wanafunzi hao, jijini hapa.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa mafunzo hayo kwa vijana wa vyuo ili kuchangamkia fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo na ufugaji ambazo zitasaidia wao kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa na serikali.

Msantu alisema baadhi ya vijana hawana uelewa kuhusu sekta hizo zinavyochangia ukuaji wa uchumi hivyo ni vema serikali ikawa na utaratibu wa kuendesha semina endelevu ambazo zitasaidia kuwajenga uwezo kwenye nyanja hizo.

"Tunaomba serikali kupitia taasisi zake iwe inaandaa semina endelevu za kuwajenga vijana, ikiwamo kuwafuatilia kile wanachofanya, ili kuwasaidia kujua namna ya kutumia fursa zilizopo nchini," alisema Msantu.

"Kuna makundi ya vijana wapo wanaelewa nini maana ya fursa, lakini makundi mengine yapo tu hayajui kitu chochote, hivyo semina hizo zikitolewa zitasaidia vijana kutambua ninii wanatakiwa wafanye ili kujiinua kiuchumi," aliongeza.

Pia alisema warsha zikiwa zinafanyika mara kwa mara hizo zitasaidia kufikisha fursa ambazo baadhi yao hawajui.

Alisema lengo lao ni kuona vijana wanatumia fursa zilizopo ili kuhakikisha wanachangia kukuza uchumi wa kati wa viwanda.

Hata hivyo, alisema taasisi hiyo imejipanga kuhakikisha vijana wanatumia fursa hizo na kuchangia pato la taifa.

Naye mshiriki wa mkutano huo, Husna Said, alishukuru taasisi mbalimbali ambazo zinazofanya jitihada za kuandaa makongamano mbalimbali ya kuwafundisha vijana namna ya kuunda vikundi kwa ajili ya kuendesha biashara.

Said alisema makongamano hayo yamesaidia kuwafumbua vijana na kutoa mwanga kufikia ndoto zao za kujikwamua kiuchumi.

"Tunaomba serikali nao wajenge utaratibu wa kuandaa warsha za kuwajenga vijana namna ya kutumia fursa wanazotoa," alisema Said.

Alisema wakifanya hivyo itawasaidia kwa kiasi kikubwa vijana wengi kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo na fursa nyingine zinazotolewa na serikali.





## Mpango waandaliwa kudhibiti ulanguzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeanzisha utaratibu mpya wa kuongeza masoko na vituo vya kuuzia mazao ya wakulima ili kudhibiti wimbi la madalali ambao wamekuwa wakiwaibia wakulima.

Ofisa Biashara wa Mkoa, Stanley Kibakaya, alisema hayo jana wakati akizungumzia hali ya masoko ya mazao mbalimbali yakiwamo mchele na mahindi ambayo bei yake si ya kuridhisha kwa mujibu wa wakulima.

Kibakaya alisema serikali imeanzisha vituo vya kuuzia mazao katika maeneo mbalimbali ambavyo vitatumiwa na wakulima pamoja na wafanyabiashara kuliko ilivyo sasa, ambapo madalali ndio hutumika zaidi na kupata faida kuliko wakulima wenyewe.

"Msimu huu wa kilimo hali ya biashara za mazao ina ushindani sana kwa sababu mazao ni mengi na wafanyabiashara ni wengi pia, hivyo kusababisha mazao kuuzwa kwa bei ambayo haimnufaishi mkulima. Kinachotakiwa sasa ni wakulima kuongeza thamani ya mazao yao ili kupata faida," alisema Kibakaya. Aidha, aliwashauri wafanyabiashara kuendelea kuhifadhi mazao kwenye maghala wakiendelea kusubiri bei ya kupanda kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

Kuhusu upatikanaji wa mafuta ya kupikia, Kabakaya alisema wanaendelea kuyafanyia kazi maagizo ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, la kutaka wafanyabiashara kuanza kuagiza malighafi hiyo nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya wananchi.Alisema wanaendelea kuhamasisha wafanyabiashara licha ya kuagiza mafuta hayo, lakini wahakikishe wanauza kwa bei nafuu ambayo kila mwananchi ataimudu.

Ofisa huyo alisema hali ya mafuta kwa mkoa wa Mbeya ni nzuri japo kikwazo kikubwa ni kuuzwa kwa bei kubwa kulinganisha na ilivyokuwa awali, hivyo akawaomba wafanyabiashara kupunguza gharama sambamba na kuacha kuficha mafuta wakisubiri kuuza kwa bei ghali zaidi. Mmoja wa wafanyabiashara wa mafuta ya kupikia katika soko la Mwanjelwa, Gasper Moses, alisema sababu iliyochangia bei ya malighafi hiyo kupaa ni uhaba wa alizeti kutoka kwa wakulima.

Alisema sababu iliyochangia alizeti kuadimika kwa wakulima ni mvua za msimu uliopita kuwa nyingi hali iliyoharibu zaidi hilo na wakulima kuvuna mazao kidogo ambayo hayajakidhi mahitaji ya soko.

# Vikosi ulinzi, usalama mguu sawa Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VIKOSI vya ulinzi na usalama mkoani Mbeya vimeanza kuzingira bonde oevu la Ihefu katika Wilaya ya Mbarali ikiwa ni maandalizi ya kuendesha operesheni ya kuondoa kwa nguvu makundi ya ng'ombe yaliyoingizwa na wafugaji kinyume cha sheria.

Hatua ya vikosi hivyo kuanza kuzingira bonde hilo inatokana na muda wa siku sita uliotolewa na serikali kwa wafugaji hao kuondoa mifugo yao kwa hiari kuelekea mwishoni.

Januari 8, mwaka huu, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, chini ya mwenyekiti wake, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ilikutana na wafugaji hao na kutoa siku sita ambazo unamalizika leo.

Pia kamati hiyo iliutaka uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutumia muda huo kutoa elimu na kuhamasisha wafugaji hao ili waondoe mifugo hiyo kwa hiari kabla vyombo vya dola kuamuliwa kutumia nguvu kuwaondoa.

Mratibu wa Operesheni Tokomeza Mifugo katika Bonde la Ihefu, Deogratius Mwageni, alisema vikosi hivyo vimejipanga kuendesha operesheni hiyo kwa njia kuu nne.

Mwageni alisema baada ya muda uliotolewa wa kuondoa mifugo kwa hiari kumalizika, viko vikosi vya jeshi vitakavyoendesha operesheni hiyo angani, majini na nchi kavu ili kuhakikisha hakuna ng'ombe hata mmoja atakayesalia ndani ya bonde hilo.

"Kuna kikosi kitatumia chopa kwa njia ya anga, pia watakuwapo askari watakaotumia boti, wengine watakwenda kwa magari na pia kipo kikosi cha askari watakaokuwa wakitembea kwa miguu. Tunaamini hakuna mfugaji yeyote atakayejificha tusimpate ndani ya bonde la Ihefu," alisema Mwageni.

Alisema tangu utolewe muda kwa wafugaji kuondoa mifugo yao kwa hiari ndani ya Bonde la Ihefu, askari wote wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) walikatazwa kuwakamata wale wanaotii amri ya kuondoa mifugo hiyo kwa hiari pale wanapokutana nao mahali popote ndani ya hifadhi.

Mwageni alisema hiyo ilikuwa fursa nzuri kwa wafugaji hao kutumia kuondoka ndani ya bonde la Ihefu na kudai kuwa yeyote atakayekaidi mpaka muda wa siku sita uliotolewa ukapita hawatakuwa na huruma naye.

Akizungumza na wananchi wakati wa kutoa elimu kwa wafugaji ili waondoe mifugo yao ndani ya Bonde la Ihefu, Mkuu wa Uhusiano na Ujirani Mwema wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Sharif Yassin, alisema katika operesheni hiyo, mifugo itakayokamatwa haitarejeshwa kwa wafugaji kama ilivyozoeleka.

Yassin Alisema katika siku za kawaida, mifugo ilipokuwa ikikamatwa ndani ya hifadhi ikiwamo Bonde la Ihefu, walikuwa wakitozwa faini na kurejeshewa mifugo yao, jambo ambalo halitafanyika wakati wa operesheni inayokuja.

"Tunasisitiza kuwa mkaiondoe mifugo yenu kabla ya kuanza kwa operesheni inayokuja, kwa sababu safari hii mifugo itakayokamatwa itataifishwa na serikali na wala suala la kulipa faini halitakuwapo, badala yake mifugo hiyo itauzwa kwa bei ambayo itaamuliwa na serikali," alisema Yassin.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Matagri Mbigili, aliwaonya wafugaji wenzake kuwa wasipuuze amri ya kuondoa mifugo yao ndani ya Bonde la Ihefu kwa madai kuwa inaweza kuwasababishia umaskini wa kudumu.

Alisema serikali haitanii katika operesheni hiyo, hivyo wafugaji wanachotakiwa kwanza ni kuondoa mifugo yao ndani ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kabla ya kufikiria mahali pengine pa kupeleka.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kuweka alama za barabarani katika barabara kuu ya Chunya na Makongolosi, mkoani Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbeya, Shinyanya vinara mfumo dume kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MIKOA ya Mbeya na Shinyanga ina idadi kubwa ya wanaume wanaowaachia wanawake pamoja na watoto shughuli za maandalizi ya kilimo, imeelezwa.

Hata hivyo, imeelezwa kuwa unapofika wakati wa mavuno, hujingilia kati na kuuza mazao hayo bila kuwashirikisha wenza wao.

Mtafiti na Mchambuzi wa Masuala ya Jinsia Tanzania, Deogratius Temba, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe juu ya adha wanazipata wanawake na watoto katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo.

Temba alisema katika mikoa hiyo, kuna wimbi kubwa la wanaume kuwaachia jukumu wenza wao kufanya shughuli zote za shamba kuanzia maandalizi, kupanda na kuvuna na kwamba yanapofika ndani wanaume hutumia mabavu kuamua kuuza mazao hayo pasipo kuwashirikisha wake zao. Alisema kitendo hicho ni cha unyanyasaji wa kijinsia kwani shughuli za kiuchumi lazima ziwahusishe mwanaume na mwanamke kuanzia maandalizi ya kilimo hadi wakati wa mavuno na kupanga kuuza kwa pamoja.

Alitaja baadhi ya sababu zinazochangia ukatili huo wa kiuchumi kuwa ni baadhi ya wanaume kuendelea mitazamo na mfume dume kwamba jukumu la kuandaa mashamba ni la mwanamke.

Kwa mujibu wa Temba, wanaume wanaofanya vitendo hivyo wanapaswa kubadilika mtazamo na kutambua kuwa ni wajibu wao kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kilimo ili rasilimali inayopatikana iwanufaishe watu wote.

Alisema ili kukomesha tabia hiyo ya wanaume kuwaachia jukumu la kilimo wanawake, Idara ya Maendeleo ya Jamii inapaswa kuendelea kutoa elimu hususani maeneo ya pembezoni ambayo ndiyo vitendo hivyo hufanyika zaidi.

"Kuna mzigo mkubwa wanawake wanabeba kuanzia maandalizi ya shamba na wanaonufaika zaidi ni wanaume. Kinachohitajika ni rasilimali za kilimo zinufaishe makundi yote ndani ya familia na itasaidia kupanga bajeti kwa pamoja na kuleta maendeleo," alisema Temba.






Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Suleiman Makame (katikati), akizungumza jijini Zanzibar jana, baada ya Mamlaka ya Maji Visiwani Zanzibar (ZAWA) na kampuni ya Tigo kuingia makubaliano, ambapo wateja wataanza kulipia maji kupitia Tigopesa. Kulia ni Mkurugenzi wa ZAWA, Mussa Ramadhani Haji na Mkuu wa Kitengo cha Fedha Tigopesa, Angelica Pesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi aongeza muda maonyesho biashara ZNZ

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, jana alitembelea maonyesho ya Saba ya Biashara Zanzibar na kuridhia ombi la wafanyabiashara la kuongezewa siku mbili zaidi ya maonyesho hayo.

Akizungumza na uongozi wa Wizara ya Biashara pamoja na Kaimu Waziri wa Wizara hiyo ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Soraga, kabla ya kutembelea maonyesho hayo, Dk. Mwinyi alisema si vibaya maonyesho hayo yakaendelea kwa siku mbili hadi keshokutwa.

Rais Mwinyi ambaye alikuwa amefuatana na mke wake, Mama Mariam Mwinyi, akiwa katika maonyesho hayo, alielezea kuvutiwa na bidhaa mbalimbali zinazouzwa na wafanyabiashara kadhaa wakiwamo wajasiriamali wa ndani na nje na kusisitiza haja ya wizara kuendelea kuwaunga mkono.

Dk. Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kuwasikiliza wajasiriamali aliowatembelea kwa niaba ya wenzao mafanikio waliyoyapata katika shughuli zao pamoja na changamoto walizo nazo.

Kutokana na maelezo hayo, Dk. Mwinyi aliwaahidi wafanyabiashara wakiwamo wajasiriamali hao kwamba changamoto zinazowakabili zitafanyiwa kazi kwa lengo la kupata mafanikio zaidi.

Mapema Waziri Soraga alimweleza Rais Mwinyi kuwa taasisi zilizoshiriki katika maonyesho hayo ni 360 zikiwamo zile za ndani na nje ya Zanzibar.

Alisema maonyesho hayo ambayo yalizinduliwa rasmi Januari 6, mwaka huu na Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, yameshirikisha taasisi 340 za wajasiriamali na 12 za kifedha.

Rais Mwinyi na mkewe walitembelea mabanda mbalimbali ya maonyesho ya biashara yakiwamo ya wajasiriamali kama vile yanayohusiana na masuala ya mwani, viatu, vifaa vya ujenzi, mazulia na ujasiriamali wa vikundivya watu wenye ulemavu.

Wafanyabiashara hao walimpongeza Dk. Mwinyi kwa hatua yake ya kwenda kuwatembelea sambamba na kumweleza changamoto na mafanikio wanayoyapata.

Maonyesho hayo ya biashara hufanywa kila mwaka katika shamrashamra za sherehe za Mapinduzi.

# Makamu Rais ahimiza ushirikiano na sekta binafsi kuleta maendeleo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema fursa nyingi zinazopatikana ndani ya sekta binafsi zinaweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa taifa endapo zitatumiwa vizuri.

Akizungumza na viongozi wa Bodi ya Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar jana, ofisini kwake, Vuga, Hemed alisema sekta binafsi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Hemed alisema kwa vile sekta binafsi inaweza kufanya vyema katika ajira, serikali imejikita kufanya kazi kwa karibu na sekta hiyo kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashara ili kuona malengo ya pande zote mbili katika ongezeko la mapato yanafanikiwa.

Aliupongeza uongozi wa bodi hiyo kwa mtazamo wake wa kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jambo ambalo limeanza kuleta faraja hasa kitendo cha kuanza kwa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Hemed aliutaka uongozi huo upungufu uliomo katika baadhi ya sheria zenye utata ili ufanyiwe marekebisho na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya washirika wa biashara.

Aliwakumbusha viongozi wa bodi hiyo kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa wafanyabiashara kulipa kodi jambo ambalo halina mjadala kwa vile ni wajibu wao kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa Hemed, wako baadhi ya wafanyabiashara wenye tabia ya kupindisha sheria zilizowekwa na badala yake kuendeleza dharau na kiburi, hivyo kusababisha wakati mwengine kutumia kisingizio cha majina ya viongozi ambao hawaelewi kama wanawachafulia heshima yao.

Kuhusu wataalamu wazawa, Makamu wa Pili wa Rais alisema azma ya serikali iko pale pale katika kuwatumia wataalamu wake kwenye miradi mbalimbali ya kiuchumi na ya kijamii.

Alisema tabia ya kuwadharau wataalamu wazalendo, mbali na kuwavunja moyo, pia inasababisha kushindwa rasimali zilizopo ikiwamo taaluma waliyopatiwa wataalamu hao.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Jumuiya hiyo, Ali Amour, alisema sekta binafsi imeshaweka mkazo wa kuona malengo yaliyomo ndani ya Dira ya Taifa ya Mwaka 2020-2050 yanafikiwa.

Alisema katika kuunga mkono hatua hiyo muhimu kwa maendeleo na uchumi, alisema bodi imeamua kubadilisha mpango kazi wake wa miaka mitatu na kusogeza mbele miaka mitano ili kwenda sambamba na kasi ya serikali.

Nguvu kubwa, alisema italenga katika uhamasishaji wa ulipaji wa kodi halali na serikali itawajibika kuendelea kujenga mazingira bora katika kuwapatia taaluma watendaji na wasimamizi wa taasisi zake ili waendelee kusimamia majukumu yao kwa uadilifu na uzalendo.

# Rais apongeza juhudi UNESCO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amepongeza azma ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na serikali kujenga jengo la Beit Al Ajaib baada ya kuanguka hivi karibuni.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, jijini Zanzibar, alipofanya mazungumzo na mwakilishi UNESCO, Tirso dos Santos.

Rais Mwinyi alimweleza dos Santos kuwa serikali inathamini uhusiano na ushirikiano uliopo kati yake na shirika hilo, hivyo hatua yake hiyo ya kulifanyia matengenezo jengo hilo ni uthibitisho tosha.

Alisema serikali ilianza kuchukua hatua za makusudi baada ya kutokea tukio hilo ikiwa ni pamoja na kuunda kamati ya uchunguzi ili kujua sababu za kuanguka kwa jengo hilo.

Rais Mwinyi aliishauri UNESCO kuyafanyia tathmini majengo yote ya Mji Mkongwe ili yasiendelee kuleta athari zaidi.

Alisema azma na utayari wa UNESCO wa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika kulijenga jengo hilo la kihistoria, ina umuhimu mkubwa katika kuurejeshea hadhi yake Mji Mkongwe ambao umo katika urithi wa dunia.

Pia alifurahishwa na azma ya shirika hilo kuwaleta wataalamu kwa awamu tatu Zanzibar ili kushirikiana na Zanzibar katika kulijenga tena jengo hilo kwa mtazamo wake wa asili na kwa kiwango bora zaidi.

Aidha, Dk. Mwinyi alimweleza mwakilishi huyo wa UNESCO kwamba serikali anayoiongoza itahakikisha inatoa ushirikiano mkubwa kwa timu hizo za wataalamu watakaokuja kufanya shughuli hiyo ikiwa ni pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya utendaji kazi wao.

Sambamba na hayo, Dk. Mwinyi alilipongeza shirika hilo kwa azma yake ya kulifanyia ukarabati jengo la sinema ya Majestic ambapo tayari nusu ya fedha za ujenzi huo kwa mujibu wa mwakilishi huyo, zimeshapatikana.

Alisema shirika hilo limeshirikiana na Zanzibar kwa muda mrefu, hatua ambayo imesababisha kuimarika kwa miradi mbalimbali ambayo UNESCO inaiunga mkono ikiwamo elimu, utamaduni na afya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG.PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## VYETI VIMEPOTEA



**ELIABU GOODLUCK MTANGO** anatangaza kupotelewa na vyeti. Cheti cha Advanced Diploma in Accountancy (ADA) chenye namba **TIA/MBY/ADA/2003/2004/496** kilichotolewa na Tanzania Institute of Accountancy **(TIA)** mwaka 2006. Master of Science in Finance & Accounting chenye namba **MSC/AF/DCC/094/T.12** kilichotolewa na Mzumbe University mwaka 2014 pamoja na Transcipt. Cheti cha NIDA chenye namba **19790912-14101-00005-24.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**Taarifa ya Polisi: DAR/OST/RB/20142/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NILE FISHNET MOTORS CO.LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** yenye namba za usajili **T 974 BFC** engine namba **1HD07E9040** chasisi namba **HDJ100011067**,yeyote atyakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/OST/RB/19312/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIKUDHANI MOHAMED HALFANI anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA COROLLA RUNX yenye namba za usajili T 301 DLA chasisi namba NZE121S105573 engine namba INZC101862 yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/CEN/RB/20649/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA FORM III**

**USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M 1984 NYONGEZA)**

**Katika mahakama MWANZO MJINI PANGANI**

**Usimamizi wa mirathi 1/2021**

**Ombi la KOMBO ALLY NYANGE
Msimamizi wa mirathi marehemu ALLY KOMBO NYANGE**

Kwa yeyote anayehusika na mirathi hii

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyu wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 29/1/2021 kabla ya huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hio
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. 7/1/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALOYCE JEREMIA SIAME** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 400 BDA** chasisi namba **FK628J520417** engine namba **6D17824189** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/GOG/RB/20867/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI**

## MAOMBI YA URAIA



**SHEPHERED KARUWA**

Shephered Karuwa, mwenye picha **PASSPORT NO EN 909844,** Mkazi wa Kata ya Mazimbu, Mkoani Morogoro, anaomba uraia kwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Nchi atokayo Zimbabwe. Kazi yake ni ***Electrical and Redier Manager Alliance One, Morogoro.*** Ameishi nchini tangu 1998, yeyote mwenye sababu kwa nini asipewe uraia atume tarifa kwa Kamishina Jenerali wa Uhamiaji **S.L.P 512 DSM.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo **PONGWE**
Usimamizi wa Mirathi **NAMBA 01/2021**
Ombi la **JOHN LEONARD MARUZUKU** kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi marehemu **LEONARD CHARLES MARUZUKU**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **11/1/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 2/JAN/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **WILFRED PHIDELIS MASSAWE** anatangaza kupotelewa Na kadi ya Gari yenye namba **T 406 DRM ISUZU TXD.**Chasis namba **TXD501686896.**Engine namba **DA 120866853.**Kwa atakaeiona Atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa **KUMB: MW/NY/RB/22123/2021.**

## MNADA WA HADHARA
## MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO YA MAGOMENI NA MAHAKAMA YA MWANZO YA KAWE NITAKUWA NA ZOEZI LA KUFANYA MNADA WA HADHARA WA KUUZA KIWANJA NA NYUMBA , MNADA WA HADHARA UTAFANYIKA WAKATI KAMA RATIBA INAVYOONYESHA.

| NA | JINA | MALI INAYOUZWA NA MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | YAH: MADAI NA: 75/2020 RANDA HOLDING LTD DHIDI YA GEOFREY ANDREW MWAKAGENDA | KIWANJA CHENYE KITALU "C" HATI NO 52043 KILICHOPO MBWENI MALINDI | 29/01/2021 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 2.. | YAH: MADAI TALAKA NA: 104/2018 RACHEL MBWANDO DHIDI YA ERICK MHAGAMA | NYUMBA ILIYOPO BUNJU "A" MTAA WA MKOANI | 03/02/2021 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 3. | YAH: MADAI TALAKA NA: 104/2018 RACHEL MBWANDO DHIDI YA ERICK MHAGAMA | NYUMBA KUBWA NA NDOGO ZILIZOPO BUNJU TEGETA MSIGANI MTAA WA NYAKASANGWE | 03/02/2021 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |

**MASHARTI YA MNADA**

- UKAGUZI UNAANZA MARA BAADA YA TANGAZO HILI.
- MNUNUZI ANATAKIWA KULIPIA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75% SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA NA HUKIKOSA KULIPA MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZOLIPA HAZITARUDISHWA.
- GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA ZA MALI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE
- MTEJA ATATAKIWA KULIPA FEDHA TASLIM SIO HUNDI.

**KWA MAWASILIANO SIMU: 0712 667989**

**OFISI ZA MATANGAZO**

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**HURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax:+255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
,Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa kampuni ya **PMM ESTATES (2001) LTD** itasafirisha mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **BANDARINI** kuelekea **PMMICD** kwa gari zenye namba za usajili **T861CVX/T550DC-C,T186DQV/T773DQV,T275DQV/T758DQV,T870CVX-/TCVZ,T192DQV/T805DQV,T209DQV/T759DQV.**
   Safari imepangwa kuanza tarehe **15.01.2021**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita** **17.5**
   **Upana - mita** **3.4**
   **Kimo - mita** **6.1**

3 Njia itakayotumika ni **MANDERA ROAD NA NYERERE ROAD.**

Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ataka sheria kuendana na kasi ya uchumi

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sufini Mchome, ameitaka Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (TUMESHERIA) kuangalia mifumo na sheria utakayoiwezesha Tanzania kuelekea uchumi wa juu kutoka katika nchi za uchumi wa kati uliopo sasa.

Akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa 15 wa Baraza la Wafanyakzi la Tume hiyo, jana, katika ukumbi wa Benki Kuu Mwanza, Prof. Mchome, alisema Tanzania haiwezekani kuwa na sheria sheria ilizo nazo Tanzania kwenye uchumi wa kati bila kuzifanyia tathmini kama inataka kwenda uchumi wa juu.

Kwa mujibu wa Prof. Mchome, wakati sekta mbalimbali kama vile viwanda na utekelezaji miradi mikubwa ya kimkakati kama vile ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) zikichukua hatua, sekta ya sheria nayo inahitaji kuangalia sheria zinazohitaji kufanyiwa maboresho kwa kuwa Tanzania ilishatoka kwenye sheria zinazokidhi uchumi maskini.

Pia aliitaka tume hiyo kuhakikisha inadhibiti ubora wa kazi zake na kuongeza kuwa mara kadhaa Rais John Magufuli amekuwa akikemea ucheleweshaji mikataba na kuongeza kuwa hata eneo la sheria kumekuwa na changamoto zisizoendana na kasi ya maendeleo.

"Sheria ina nafasi yake na isipotekelezwa vizuri, tutakwamishana. Kwa hiyo mitazamo na kazi kubwa tunayotakiwa kwenda nayo kama tume ni kujiimarisha. Huwezi kwenda bila kujitathmini, " alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa TUMESHERIA, Casmir Kyuki, alisema pamoja na mambo mengine, imekuwa ikifanya tathmini ya sheria mbalimbali na kupendekeza hatua za kuchukua serikalini kwa lengo la kuleta ufanisi kwenye sekta ya sheria.

Kyuki aliongeza kuwa kwa sasa inachofanya tume yake katika masuala ya sheria ni kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo na kusisitiza kuwa sekta ya sheria inatakiwa kuisaidia nchi kwenda mbele.

Benki ya Dunia Julai Mosi, mwaka jana, iliorodhesha Tanzania katika orodha ya nchi za uchumi wa kipato cha kati, hatua ambayo imefikiwa miaka mitano kabla ya Dira ya Maendeleo ya Taifa iliyoilenga kuifikisha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025.



Mtumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mariana Mahwaya, akimhakiki Mzee mstaafu Theones Rutehangwa, mkazi wa Mkoa wa Mwanza, wakati wa zoezi la uhakiki wastaafu wanaolipwa pensheni moja kwa moja na Hazina, katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza jana. **PICHA: WFM**

# Wastaafu wamiminika kuhakikiwa

**Na Josephine Majura, MWANZA**

WASTAAFU wanaolipwa pensheni zao na Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina), wamejitokeza kuhakikiwa katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Geita, ikiwa ni mkakati wa serikali wa kuhuisha taarifa za wastaafu hao.

Akizungumza jijini hapa, mratibu wa zoezi hilo, ambaye ni Mhasibu Mkuu sehemu ya pensheni kutoka Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango, Scola Mafumba, amesema kuwa uhakiki huo umelenga kuhuisha taarifa za wastaafu hao na kuziweka kwenye mfumo wa kielektroniki.

Alisema zoezi hilo lilianza rasmi Desemba 7, 2020 na linatarajiwa kukamilika Machi, mwaka huu, mpaka sasa wastaafu katika mikoa 10 ya Tanzania Bara wamehakikiwa na litafanyika hadi Zanzibar.

"Baada ya hapa tutaelekea mikoa ya Shinyanga, Mara na Simiyu kuanzia tarehe 18 Januari, 2021 ambapo kazi tunayoifanya ni kuhakiki na kukusanya taarifa za wastaafu na kuziweka kitaalamu ili kuboresha kanzidata ya wastaafu iliyoko Hazina," alisema Mafumba.

Alisema uhakiki huo ni lazima kwa wastaafu wote na kuongeza kuwa ambao hawatahakikiwa wataondolewa kwenye orodha ya malipo ya pensheni kuanzia Aprili, 2021.

Aliwaasa wastaafu kujiepusha ama kujihadhari na matapeli wanaowarubuni kwamba watawasaidia kupata pensheni zao na kuwadai rushwa na kuwa huduma za wastaafu zinatolewa bure na serikali.

"Kama kuna mstaafu anataka kupata taarifa zozote zinazohusu mafao yao tunawashauri wafike kwenye ofisi za Hazina ndogo zilizoko mikoa yote nchini na kamwe wasikubali kutoa fedha zao kwa mtu yeyote kwa sababu huduma za wastaafu zinatolewa bure na serikali," alisisitiza Mafumba.

Wastaafu hao wameipongeza serikali kwa hatua wanayochukua ya kuwahakiki na kuboresha taarifa zao ambazo zitakuwa zikipatikana mahali popote kwa njia ya mtandao.

Pia wameomba serikali kuwaongezea pensheni wanayolipwa kila mwezi ili waweze kukabiliana na changamoto za maisha zinazowakabili ikiwamo afya.

# Bil. 5.8/- kutekeleza miradi ya maji Songea

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WILAYA ya Songea mkoani Ruvuma inatarajia kutumia Sh. bilioni 5.799 kutekeleza miradi minane ya maji katika kipindi cha mwaka 2020/21.

Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Songea, Mhandisi Mathias Charles, alisema jana kuwa hadi sasa RUWASA imepokea zaidi ya Sh. milioni 877 sawa na asilimia 15.12 ya bajeti iliyopangwa.

"Hadi kufikia Januari 2021, wakazi wanaopata huduma ya maji Wilaya ya Songea wanakadiriwa kuwa 132,362 sawa na asilimia 63.6 ya wakazi wote," alisema Charles.

Alisema hadi sasa mamlaka hiyo imetumia zaidi ya Sh. bilioni tatu kutekeleza miradi tisa ya maji katika wilaya hiyo na kwamba RUWASA inaendelea na uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji kwa kujenga miradi mipya.

Charles aliitaja miradi ya maji iliyopangwa kutekelezwa katika Halmashauri ya Madaba kupitia P4R kuwa ni Ndelenyuma, Lutukira na Mbangamawe kupitia PBR4 mradi mmoja wa maji katika kijiji cha Igawisenga unatarajia kutekelezwa.

Meneja huyo alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, kupitia P4R, miradi ya maji inatarajia kutekelezwa katika vijiji vya Lipaya, Lundusi na Maposeni na kupitia PBR4 mradi mmoja unatarajia kutekelezwa katika kijiji cha Ndongosi na mwingine kutekelezwa Ndilimalitembo Manispaa ya Songea.

Kwa mujibu wa meneja huyo, RUWASA inaendelea kukarabati miradi iliyokuwa imechakaa na kuboresha usimamizi wa miradi iliyokamilika ili iwe endelevu kwa kuunda na kusajili jumuiya za watumiaji maji (CBWSO) ambazo zitakuwa zinasimamia miradi hiyo na kuhakikisha inatoa huduma wakati wote.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2019/20 RUWASA ilipanga kuunda na kusajili jumuiya za watumiaji maji 17 na hadi Juni, 2020, mwaka jana, jumuiya 10 zilikuwa zimeundwa na kusajiliwa.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, jumuiya 28 zilipangwa kuundwa na kusajiliwa na kwamba hadi sasa jumuiya 11 zimeundwa. Alisema RUWASA Songea imepanga kukamilisha usajili wa jumuiya za watumiaji maji ifikapo Juni 30, mwaka huu, na wamejipanga kuendelea kutoa elimu juu ya utunzaji vyanzo vya maji na elimu kuhusu umuhimu wa ulipaji wa huduma za maji, ili kuifanya miradi iwe endelevu.



# TIMOTHY

## FOSU-MENSAH ATUA LEVERKUSEN

**MUNICH, Ujerumani**

MLINZI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Timothy Fosu-Mensah, amejiunga na klabu ya Bayer Leverkusen.

Hata hivyo, kwa mujibu wa BBC Sport dili hilo halijawekwa wazi kama ni uhamisho wa mkopo au wa kudumu.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 23 alitokea kwenye akademi ya Ajax kabla ya kujiunga na United kwenye timu ya vijana mwaka 2014.

Mechi yake ya kwanza kwa Mashetani Wekundu hao ilikuwa mwaka 2016, lakini kabla ya hapo alitumika kwa kucheza kwa mkopo katika klabu ya Crystal Palace na Fulham ambapo kwa ujumla amecheza mechi 30 ndani ya Old Trafford.

Leverkusen ilithibitisha kwenye tovuti yake kuwa imemsajili Fosu-Mensah bila kutoa maelezo zaidi.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

# CONTER: INTER IMESTAHILI KUTINGA FAINALI

**MILAN, Italia**

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte amesisitiza timu yake ilistahili kwa sifa zote kabisa kutinga fainali ya Coppa Italia na walikuwa na nafasi ya kuwachapa Fiorentina katika muda wa kawaida wa mchezo huo wa Jumatano.

Hata hivyo, Inter walihitaji hadi dakika 118, ambapo Romelu Lukaku aliwatoa kimasomaso kwa bao la kichwa na la ushindi, baada ya penalti ya Arturo Vidal na mkwaju wa Christian Kouame kumaliza dakika 90 kwa sare ya 1-1.

"Tulistahili kufuzu, na ilitakiwa kuwa ndani ya dakika 90 za awali, kwa sababu tulikuwa na nafasi kubwa ya kushinda. Vijana walifanya vyema, kucheza dakika 120 wakiwa vyema na kujipanga kwa usawa. Nimeridhika," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari.

"Ilikuwa lazima tushinde na kwa hakika kabisa hiyo tulistahili, ingawa ushindi ulilazimika kusubiriwa kwa muda, lakini hatimaye tulipata tulichokuwa tunakitaka.

Conte amebainisha kuwa amefurahi wachezaji wale ambao walikosa nafasi ya kucheza kwa muda mrefu kwa sababu tofauti, kama Aleksandar Kolarov na Andrea Ranocchia walivyothibitisha ni kwa namna gani wanaijali Inter.

Conte anaamini kuwa alikuwa na kikosi bora zaidi kufuatia uchaguzi alioufanya, na kilistahili kupata matokeo mazuri na kufanikiwa.

# MADRID YAMFUNGIA KAZI MBAPPE

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid iko tayari "kumpandia dau Kylian Mbappe" na wako tayari kulipa pauni milioni 200.

Mpango wa muda mrefu wa Real Madrid wa kumnasa Mbappe kutoka Paris Saint-Germain unaweza kuwa mzuri wakati wa majira ya joto kwa mujibu wa chapisho la gazeti la Hispania la AS, lilibeba kichwa cha habari "Operesheni Mbappe".

Na kwa mujibu wa ripoti hiyo ya AS, Real Madrid wanakaribia kukamilisha mpango huo na kuna uwezekano mkubwa wa kuinasa saini ya nyota huyo kipindi cha majira ya joto kijacho.


Mkataba wa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa kule PSG unamalizika Juni, mwaka 2022, hivyo umebaki mwaka mmoja.

Hadi sasa Mbappe hajaonyesha nia ya kutaka kusaini mkataba mpya na miamba hao wa jiji la Paris.

Miamba hiyo ya Hispania inaamini ada ya kumsajili Mbappe inaweza kuwa kati ya euro milioni 150 hadi milioni 222.

Kwa mujibu wa ripoti, PSG inataka kuiga walicholipa kumsajili Neymar kutoka Barcelona mnamo mwaka 2017.





# BARCA

## YAJITOSA KWA AGUERO

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona inahusishwa na mpango wa kumsajili nyota wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero kwa mujibu wa vyanzo vya habari za michezo kutoka Uingereza.

Mkataba wa nyota huyu kwa sasa na City unaisha Juni 30, mwaka huu na baada ya hapo atakuwa mchezaji huru, anaweza kutia saini na timu yeyote.

Barcelona wanatajwa kuwa wanahitaji huduma yake baada ya kumalizana na Manchester City.

Barca wanaingia kwenye ushindani na Paris Saint-Germain ya Mauricio Pochettino ambao pia wanatajwa kuiwinda kwa ukaribu zaidi huduma ya nyota huyo.

Aguero kwa sasa amejiweka karantini kwa siku 10 baada ya kupatikana na maambukizi ya virusi vya corona.

Nyota huyo amekuwa taswira muhimu kwenye soka la England na kutoa mchango mkubwa City, pia ana urafiki wa karibu sana na Lionel Messi, na huenda hii ikawa inataka kutumika kama mbinu ya kumbakiza Messi katika kikosi cha Barcelona.

# CITY, JUVE ZAMGOMBEA LOCATELLI

**MANCHESTER City**

KLABU ya Manchester City imeripotiwa kuwa kwenye mbio moja na Juventus kuwania saini ya kiungo wa Sassuolo, Manuel Locatelli anayetajwa kuwa na thamani ya euro milioni 35.

Nyota huyo ambaye ni zao la akademi ya soka ya vijana ya Milan amefikisha umri wa miaka 23 wiki iliyopita, na mpaka sasa tayari ameshacheza mechi sita za Timu ya Taifa ya Italia.

Juventus hawakuweka siri juu ya malengo yao ya kumtaka Locatelli, ambaye amecheza jumla ya mechi 126 za Serie A hadi sasa akiwa na mabao sita na pasi za mwisho tisa.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, pia jicho la Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola limetua kwa nyota huyo.

Wakala wake, Stefano Castelnuovo alinukuliwa akisema; "Tuna uhusiano mzuri sana na Sassuolo, klabu ina mipango mikubwa sana. Tutaona nini kitatokea, kama ofa nzuri ikija, itakuwa ni heri kwa kila mmoja kufikia makubaliano.

"Lakini wakati wote tutawashukuru Sassuolo. Atawashukuru Milan wakati wote, lakini nadhani atakuwa anatafuta changamoto mpya, Italia au nje ya Italia. Ana ndoto ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, bila shaka yeye na Sassuolo watapata zawadi msimu wa joto.





# POCHETTINO ABEBA TAJI LA KWANZA PSG

**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino kwa mara ya kwanza amebeba kombe kwenye maisha yake ya kuwa kocha.

Raia huyo wa Argentina ameondoa ukata huo baada ya PSG kuwaburuza Marseille usiku wa kuamkia jana na kulibeba kombe.

PSG walikuwa wakichuana na Marseille kwenye fainali ya kombe hilo ukiwa ni mchezo wa tatu kwa Pochettino tangu akabidhiwe kikosi cha timu hiyo.

Trophee des Champions ni kama kombe la Ngao ya Hisani la Ligi Kuu England, EPL, ukimkutanisha bingwa wa ligi dhidi ya bingwa wa kombe la ligi kwa msimu uliopita.

Mabao ya Mauro Icardi na Neymar Jr yaliwatosha PSG kuwazidi kete Marseille licha ya Dimitri Payet kupachika bao la kufutia machozi.

Ushindi kwa PSG umeendeleza umwamba wa timu hiyo kwenye soka la Ufaransa, hili linakua kombe la 19 kati ya 20 ambayo PSG wamecheza hatua ya fainali kwenye mashindano ya ndani.

Hii ni mara ya nane mfululizo kwa PSG kubeba taji la Trophee des Champions.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA HATIHATI KUMKOSA MESSI

●●●Ni katika fainali ya mashindano ya Supercopa inayotarajiwa kuchezwa Jumapili kutokana na...

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Ronald Koeman, amesema hana uhakika kama Lionel Messi atakuwapo kwenye mchezo wa fainali ya Supercopa de Espana utakaochezwa Jumapili.

Messi aliukosa mchezo wa Jumatano ambao Barca walishinda kwa mikwaju ya penalti kwenye nusu fainali ya kombe hilo dhidi ya Real Sociedad kwa sababu ya kutokuwa kwenye hali nzuri kiafya.

Marc-Andre ter Stegen aliokoa penalti mbili wakati Barca wakipata tatu dhidi ya mbili za Sociedad baada ya mchezo kumalizika kwa sare ya bao 1-1 kwenye dakika za kawaida.

Fainali hiyo inaweza kuwakutanisha na Real Madrid au Athletic Bilbao waliokuwa wanacheza jana kwenye hatua ya nusu fainali ya pili.

Koeman amesema bado hana uhakika kama Messi atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo huo.

"Kwanza najisikia fahari kubwa na timu hii, kwa sababu kama ukihesabu wachezaji wote wanaokosekana kwa sasa, nafikiri ni muhimu kuwa na watu nyuma ambao wanaweza kusaidia. Nafikiri leo tulitimiza kwa kila njia," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari.

"Najua Real (Sociedad) walikuwa na nafasi zao kama sisi. Tuliweza kushinda baada ya penalti.

"Kuhusu Leo, lazima tusubiri kwa siku chache zijazo kujua kama atakuwapo kucheza fainali hii."

Frenkie de Jong aliwaweka mbele Barca kabla ya Sociedad kusawazisha kupitia Mikel Oyarzabal katika kipindi cha pili.

## KWA UFUPI

**LINGARD ANUKIA NICE**

WAWAKILISHI wa kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard (28), wamefanya mazungumzo ya awali kuhusu uhamisho wake wa mkopo kwenda Nice, lakini mazungumzo rasmi yakitarajiwa kufanyika wiki ijayo. ***(Sky Sports)***

**ASHLEY AMBEBA BRUCE**

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anaungwa mkono na mmiliki wa klabu hiyo, Mike Ashley, licha ya shinikizo kutoka kwa mashabiki wanaotaka afutwe kazi kutokana na mwenendo mbaya wa timu. ***(Sky Sports)***

**TRIPPIER AKWAMA**

MANCHESTER United wamesitisha mpango wa kumnunua mlinzi wa kushoto wa Atletico Madrid, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30 mwezi huu. ***(Manchester Evening News)***

**SPURS KUMTEMA ROSE**

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikafutilia mbali mkataba wa Danny Rose katika dirisha la uhamisho la Januari hii, huku West Brom ikionyesha azma ya kutaka kumnunua beki huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Talksport)***

**OZIL SAFARI IMEIVA**

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, ameamua kuacha pauni milioni saba alizotarajiwa kupokea kabla ya mwisho wa msimu huu, ili afanikiwe kukatiza mkataba wake na kuondoka mwezi huu. ***(The Athletic)***

**GRACIA, BARCA SAFI**

MLINZI wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 20, amefikia makubaliano kibinafsi na Barcelona, lakini uhamisho wake haujakaribia kukamilika. ***(Goal)***

**WIJNALDUM KUTUA BARCA**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, ana imani ya kumsajili kiungo wa kati wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, na mshambuliaji wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay mwenye miaka 26 kwa mkopo mwezi huu. ***(Mundo Deportivo)***

**BOLOGUN AKARIBIA RB**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 19 ambaye ni raia wa England, amekubali kujiunga na RB Leipzig ya Ujerumani. ***(Football Insider)***

**LIVERPOOL YAMFUATA WHITE**

LIVERPOOL wanajiandaa kumnunua mlinzi wa Brighton, Ben White ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Liverpool Echo)***

**NUNO ASAKA TIMU**

WAKALA wa kocha wa Wolverhampton Wanderers, Nuno Espirito Santo anatafuta timu mpya kwenye Ligi Kuu England kwa ajili ya raia huyo wa Ureno, ambaye alisaini mkataba mpya pale Molineux, September mwaka jana.***(Sun)***

**MOURINHO: WINKS HAUZWI**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesisitiza kiungo wa England, Harry Winks mwenye umri wa miaka 24, hatauzwa au kuondoka klabuni hapo kwa mkopo mwezi huu. ***(Football London)***

## HABARI MICHEZO

# SBL YAMWAGA BARAKA STARS IKIELEKEA CHAN

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA na matumaini makubwa ya kufanya vyema, Timu ya Taifa (Taifa Stars), iliondoka nchini jana asubuhi na kuelekea Cameroon kwa ajili ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zinazotarajiwa kutimua vumbi kuanzia keshokutwa.

Chini ya udhamini wa Bia ya Serengeti, Taifa Stars ipo Kundi D pamoja na Zambia, Namibia na Guinea na kikosi kimeahidi kuwapa raha Watanzania.

Mwaka jana, Bia ya Serengeti Premium Lager iliingia mkataba wa miaka mitatu na TFF na kuwa mdhamini mkuu wa Taifa Stars kwa makubaliano ya kutoa kiasi cha shilingi bilioni 3 katika kipindi cha mkataba. Mkataba huo unafuatia kumalizika kwa mkataba wa wali ambao pia ulikuwa ni wa miaka 3 uliosainiwa mwaka 2017.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema shirikisho hilo limejipanga kufanya kila liwezalo kuhakikisha mikakati ya benchi la ufundi inatekelezwa vyema ili kuiwezesha timu hiyo kufanya vyema katika fainali za CHAN.

Akizungumzia kuhusu ushiriki wa Taifa Stars katika mashindano hayo, Mkuu wa Kitengo cha Bia ya Serengeti, Anitha Msangi, alisema hana shaka na kikosi cha timu hiyo na anamatumaini itapeperusha vyema bendera ya taifa na kuongeza kinywaji cha Serengeti kama mdhamini inaitakia kila la heri.

Akiishukuru Serengeti, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema fedha zilizotolewa kwa ajili ya udhamini huo zitatumika kama ilivyokusudiwa na kuongeza zinasaidia katika kufanikisha uendeshaji ya timu na hivyo kupata matokeo mazuri kwenye michezo yake.

Akizungumza wakati wa utiaji saini wa mkataba huo mpya uliofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema bia ya Serengeti ni mdau mkubwa wa michezo hapa nchini na kuongeza imekuwa ikijivunia kuwaunganisha Watanzania kupitia michezo.

Mkurugenzi huyo aliongeza, "Tumeamua kusaini tena mkataba huu baada ya kuridhishwa na maendeleo pamoja na mafanikio ya timu kwa miaka mitatu iliyopita, lakini kutoka na mapenzi makubwa ya Watanzania kwa timu yao ya taifa."

Ikiwa ni sehemu ya kujiandaa na fainali za CHAN, Stars iliyoko chini ya Etienne Ndayiragije anayesaidiwa na Juma Mgunda na Suleiman Matola ilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mapema wiki hii iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Stars imefuzu kucheza CHAN baada ya kuisambaratisha timu ya taifa ya Kenya Harambee Stars kwa bao 4-1 jijini Nairobi baada ya mechi ya kwanza iliyofanyika jijini Dar es Salaam, ambapo timu hizo mbili zilitoka 'draw' ya bila kufungana.




Kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), pamoja na viongozi wa timu hiyo wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere kabla ya kuanza safari ya kuelekea Cameroon katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# Jackson Group, GBS kuwabeba mabondia

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wanaendeleza vipaji vya mabondia wa hapa nchini, Kampuni ya Jackson Group na Taasisi ya kimataifa inayoshughulika na ngumi za kulipwa ya Global Boxing Stars (GBS), zimesaini mkataba maalumu ambao utawasaidia wachezaji wa mchezo huo.

Moja ya fursa hizo ni kuonekana nchi nyingi duniani kupitia ushirikiano wa kampuni hizo mbili ambapo mapambano yao yataonyeshwa na washirika wengine wa GBS.

Mabondia wa kwanza kufaidika na fursa hiyo ni pamoja na Ibrahim Class ambaye atazichapa na Dennis Mwale kwenye pambano la ubingwa wa mabara wa WBF lililopangwa kufanyika Januari 29, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Next Door Arena ambao umepewa jina la GBS and Jackson Group Fight Night.

Usiku huo pia utakuwa na mapambano mengine saba ya utangulizi, Mkurugenzi wa GBS, Jeremy Bean, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana na kuongeza mabondia wa Tanzania watapata fursa ya kushiriki katika mapambano makubwa ya ngumi za kulipwa duniani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jackson Group, Kelvin Twissa, alisema wamedhamiria kuleta maendeleo makubwa katika mchezo wa ngumi za kulipwa nchini.

Twissa alisema aliposema lengo lao ni kubadili mwonekano wa mchezo wa ngumi za kulipwa kama kampuni yake ilivyoahidi na ushirikiano wao na GBS ni mwanzo wa mwelekeo mpya wa ngumi za kulipwa.

"Tumedhamiria kuleta maendeleo makubwa na ndiyo maana sasa tumeingia makubaliano na GBS, kuna mambo mengi mazuri yanakuja katika ngumi za kulipwa na naamini tutafikia lengo letu," alisema Twissa.

## Azam FC kubakia Z'bar ikijiimarisha

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

LICHA ya timu yao kuondolewa mapema katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, kikosi cha Azam FC kitaendelea kubakia visiwani humo kikiendelea kujinoa kwa ajili ya mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Kocha Mkuu wa Azam FC, George Lwandamina, aliliambia gazeti hili ameamua kuweka kambi Zanzibar kwa sababu anaamini kuna utulivu ambao utawasaidia wachezaji wake kufikia malengo.

Lwandamina alisema kambi hiyo itakuwa ya siku 10 na wanatarajia kucheza mechi tatu za kirafiki na timu za visiwani humo.

Kocha huyo alisema bado hajafahamu wapinzani watakaocheza nao, lakini anatarajia michezo hiyo ya kirafiki kuchezwa kuanzia Januari 15 na 20, mwaka huu.

"Tutakuwa huku kwa muda wa siku 10 na tutacheza mechi za kirafiki, ili kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika michuano ya Kombe la Mapinduzi, zitatusaidia kujiimarisha kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Lwandamina.

Aliongeza mipango yake kwa sasa ni kufanyia kazi upungufu wa kikosi chake ili ligi itakaporejea wawe katika ubora wa hali ya juu.

## Maadhimisho Meza kufanyika Aprili 6

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mpira wa Meza Tanzania (TTTA), kinatarajia kufanya maadhimisho maalumu ya mchezo huo ifikapo Aprili 6, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu wa (TTTA), Leonard Liunda, alisema maandalizi kwa ajili ya maadhimisho hayo yanaendelea vizuri na wanaamini yataleta mapinduzi katika mchezo huo.

"Kwa sasa tunajiandaa na shughuli kubwa ya kuadhimisha siku ya chama chetu kidunia, maandalizi yanaendelea vizuri na tumewaandalia wadau taarifa zitakazotujenga wote kwa pamoja," alisema Liunda.

Katibu huyo alisema wanatarajia timu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani zitashiriki katika maadhimisho hayo na wanatarajia kuona ushindani.

Alisema kwa sasa mchezo huo umekuwa kwa kiasi kikubwa tofauti na ukilinganisha na miaka ya nyuma iliyopita kutokana na idadi ya wanaojitokeza kuucheza katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Kipindi cha nyuma mchezo huu ulikuwa haupendwi na watu wengi walikuwa wanajua ni mchezo unaochezwa na watu wenye kipato, lakini fikira hizo sasa hazipo na watu wa aina zote wanacheza," alisema Liunda.

# Michezo

Ijumaa Januari 15, 2021

Nipashe




## BARCA HATIHATI KUMKOSA MESSI

HABARI UK 22




Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdallah Ulega (kulia), akimkabidhi nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), John Bocco, fedha kwa ajili ya posho na motisha ya kikosi hicho ambacho tayari kimeshatua Cameroon ili kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN). **PICHA: MTANDAO**

## SERIKALI YAMWAGA MAMILIONI STARS

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imekabidhi Sh. milioni 60 kwa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kwa ajili ya kusaidia posho kuelekea katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazofanyika Cameroon kuanzia kesho, imefahamika.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, alikabidhi fedha hizo juzi usiku kwa ajili ya posho ya wachezaji walipokuwa hapa nchini na motisha ya mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Ulega alisema serikali itaendelea kupambana kupata fedha kwa lengo la kusaidia mahitaji mengine ya timu hiyo inayokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye fainali hizo.

Alilitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kusimamia vyema nidhamu ya wachezaji wa timu hiyo, ili waende kufanya vizuri katika fainali hizo ambazo wanashiriki kwa mara ya pili.

"Serikali imechangia zaidi ya Sh. milioni 60 kama 'bonasi' na posho za ndani kwa wachezaji na benchi la ufundi, bado tunapambana kupata fedha za kusaidia katika maeneo mengine, TFF (Shirikisho la Soka Tanzania), hakikisheni mnasimamia nidhamu na matumizi ya fedha hizi," alisema Ulega.

Taifa Stars iliyoondoka nchini jana itaanza kutupa karata zake katika fainali hizo Januari 19, mwaka huu, dhidi ya Zambia na itashuka tena dimbani Januari 23 kuwavaa Namibia, huku mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi itachezwa Januari 27, mwaka huu dhidi ya Guinea.

# KAZE: TULIISHIKA SIMBA

## ●●●Lakini awataja Chama, Miquissone chanzo Wekundu wa Msimbazi kushindwa kutamba katika...

**Na Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, akisema kukosekana kwa kiungo, Clatous Chama na Luis Miquissione kulisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola amesema uchovu waliokuwa nao wachezaji wake uliwanyima ushindi.

Yanga ilitwaa ubingwa wa mashindano hayo kwa mwaka huu kwa penalti 4-3, baada ya kutoka suluhu katika dakika 90 za kawaida kwenye mchezo huo wa fainali uliochezwa juzi usiku.

Akizungumza na gazeti hili baada ya fainali hiyo, Kaze alisema mchezo huo ulikuwa mzuri na wenye ushindani mkubwa kwa wakati wote.

Kaze alisema wachezaji wake walicheza kiufundi na kimbinu zaidi katika dakika zote 90 na anaamini kutokuwapo kwa Chama na Miquissione imewasaidia kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Kocha huyo alisema kutokuwapo kwa nyota kuliwasaidia 'kuishika' Simba katika eneo la kiungo na pembeni kutowapa nafasi ya kupeleka mipira kwa washambuliaji wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nyota hao wawili ni hatari sana wakiwapo katika kikosi, lakini niliwaambia wachezaji wangu kutoruhusu Simba kupiga krosi." Kwa sababu kama wangeruhusu kupiga krosi na ingemfikia, Meddie Kagere nina imani ingekuwa hatari, maana ninavyomjua ni hatari kwa mipira ya vichwa," alisema Kaze.

Alisema pia kombe walilolipata ni zawadi kwa wanachama na mashabiki wa Yanga ambao kwa muda mrefu hawajachukua kombe lolote, hivyo ni haki yao washangilie.

"Wana-Yanga wamebezwa sana na wamekuwa wanyonge kwa muda mrefu. Hawajachukua kombe lolote kwa muda sasa, kwa hiyo hili kombe ni lao na wanastahili kushangilia," Kaze alisema.

Kocha huyo raia wa Burundi alisema kwa sasa anaitengeneza timu yake iwe na ari ya ushindi, na iwe inacheza mechi bila kujali mazingira yoyote.

"Nataka tucheze bila kisingizio cha mvua, jua, uwanja mbovu, sijui nini. Nataka niwe na kikosi ambacho hakitokuwa na kisingizio, tukifungwa basi tunajua ni sababu ya kiufundi," alisema Kaze.

Naye Matola alisema mechi walizocheza mfululizo wachezaji wake zimewaathiri na baadhi yao kulazimika kuwatumia katika mchezo huo wa fainali huku wakiwa majeruhi. "Tunawapongeza Yanga, wametwaa ubingwa kwa kutufunga kwa penalti, mfululizo wa mechi umetuathiri maana wachezaji wangu ikiwamo Hassan Dilunga na Miraji Athuman wakilalamika maumivu, fatiki waliyokuwa nayo imechangia kutochukuwa ubingwa," alisema Matola.

Aliongeza baada ya matokeo hayo wanarejea nyumbani na kupumzika kwa muda wa siku saba na baadaye watarejea kwa ajili ya maandalizi ya mechi za Ligi Kuu Bara na za michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi itakayoanza mwezi ujao.

Hata hivyo, Matola alisema waamuzi wa mechi hiyo walishindwa kuumudu mchezo huo wa kuacha kutoa uamuzi pale nyota wake wanapofanyiwa madhambi na wachezaji wa Yanga.

Simba na Yanga tayari zimesharejea jijini Dar es Salaam, lakini Azam FC yenyewe imebakia Zanzibar kwa ajili ya kuweka kambi ili kujiimarisha na hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaanza tena mapema mwezi ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002